# Nipashe

Jumamosi Machi 13, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580518

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII



www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**Radi** ilivyoua wanafunzi wa familia moja

UKURASA 3



**Ofisa** ardhi mbaroni tuhuma za kujipatia mil. 95/- kitatanishi

UKURASA 3



**Guardiola atajwa kocha bora zaidi**

UKURASA 21



# Ukweli aliko Rais Magufuli

UKURASA 2



Wanafunzi wa darasa la pili katika Shule ya Msingi Samilo, Kata ya Mahembe, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, wakisomea chini ya miti ya michikichi kutokana na upungufu wa madarasa shuleni hapo, jana. **PICHA: PENDO THOMAS**

## Zuio mahindi Kenya laliza vigogo wa biashara

UKURASA 2

## Wanafunzi madarasa matatu wasomea chini ya michikichi

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play

Download on the App Store



**MICHEZO** GOMES AGEUKIA MABEKI SIMBA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza baada ya kushiriki katika Sala ya Ijumaa kwenye Msikiti wa Ijumaa, Njombe mjini, jana. **PICHA: OWM**

# Ukweli aliko Rais Magufuli

**Na Romana Mallya**

KWA takribani wiki moja sasa, kumekuwa na taarifa kwenye mitandao ya kijamii zikidai Rais John Magufuli ni mgonjwa na amesafirishwa kwenda jijini Nairobi, Kenya kwa ajili ya matibabu ya kibingwa.

Taarifa hizo zilizonukuliwa na kuripotiwa na baadhi ya vyombo vya habari vya kimataifa, zilikwenda mbali zaidi zikidai kuwa Rais Magufuli sasa amehamishiwa India kwa ajili ya matibabu ya kibingwa zaidi.

Hata hivyo, taarifa ambazo Nipashe ilizipata jana asubuhi kutoka chanzo cha kuaminika, zilibainisha kwamba Rais Magufuli yupo nchini na anaendelea na majukumu yake.

Baadaye jana mchana, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, aligusia suala hilo alipozungumza kwenye Msikiti Mkuu wa Njombe akisema kuwa Majaliwa yuko mkoani Njombe kwa ziara ya kikazi.

Majaliwa aliwataka Watanzania kupuuza kuhusu alichokiita upotoshi unaoendelea kwenye mitandao ya kijamii unaoleta taharuki kuhusu afya ya Rais Magufuli, akisisitiza kuwa yupo timamu na anachapa kazi.

"Katika hili, ninataka kuonyesha baadhi ya masikitiko yangu kwa baadhi ya Watanzania ambao hawapendi maendeleo yetu, wamejawa na chuki tu! Wamejawa na husuda tu na kutaka kushuhudia taifa hili likiporomoka na kutamani kuwachonganisha Watanzania.

"Kuanzia juzi (Jumatano) na leo (jana), tena hawako ndani ya nchi, wako huko wanashawishi vyombo vya kimataifa viseme Rais wa Tanzania anaumwa, kajifungia. Wapo huko, hawapo hapa, tuliopo ndani tupo kimya, husuda tu!

"Wengine tunawajua baba zao na mama zao, wadogo zao wapo hapa na wanaona fahari kuisema nchi yao wakiwa huko," Majaliwa alisema.

Majaliwa aliwataka Watanzania watulie na kuwahakikishia kwamba uongozi wao upo.

"Mlimpigia kura nyingi Rais Magufuli, anaendelea vizuri, ameunda serikali yake na tunaona mafanikio katika nchi.

"Kumzushia ugonjwa ni chuki. Inasaidia nini? Wanasema atoke, atoke aende wapi? Aje nje, afanye nini? Mmeshamkuta anazurura Kariakoo Rais? Ushamkuta Magomeni anazunguka?" Majaliwa alihoji. Majaliwa alisema Rais ana mpango wa kazi, siyo mtu wa kuzurura, akikumbusha kuwa itifaki hiyo ya serikali inajulikana kwa wote.

"Baada ya Rais, ana msaidizi wake, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, mawaziri, wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, maofisa tarafa, watendaji wa kata mpaka kijijini.

"Nani hajui wiki mbili zilizopita Rais alikuwa anafanya kazi kubwa Chato? Alipotoka Chato, kapita Nyakanazi, Biharamuro, Kahama amefanya ziara siku tatu. Kaenda Tabora, akapita Nzega, kaenda Dodoma, akaenda Dar es Salaam.

"Azunguke mwaka mzima? Ni wakati wake wa kufanya kazi ofisini. Acha sisi tufanye kazi, ndiyo maana tupo hapa.

"Nani aliyepata bahati ya kwenda ofisini kwake (Rais) kumpiga picha akiwa anapitia mafaili?

"Kwanza, unaingiaje kwenye lile geti la Ikulu? Sasa, usipomwona, asipoita watu ndo anaumwa? Lazima kwanza tuipende nchi yetu. Pili, tuwapende viongozi waongoze vizuri nchi yetu.

"Tatu, sisi huku lazima tuzungumze lugha ya upendo, tuhamasishane, tuwe na mshikamano, tuondoe chuki kwa mtu mmoja mmoja. Wenye chuki hawatufai kwenye jamii yetu," alisema.

Majaliwa aliwataka Watanzania kuliombea Taifa, akibainisha kuwa hata jana asubuhi alipokuwa anatoka Dodoma, alimpigia simu Rais Magufuli na kumjulisha ratiba yake na kiongozi huyo wa nchi akamtuma awasilishe salama kwa wananchi wa Njombe.

"Ninaomba nirudie kwa salamu alizotupa leo (jana) kwenu wana Njombe. Mheshimiwa Rais anawasalimia sana wana Njombe, anawashukuru wana Njombe, mwaka jana mlipiga kura nyingi, na katika upigaji kura kila mmoja alikwenda kwa uhuru wake.

"Nimesema hili ili kuwatia faraja Watanzania kuwa Rais Magufuli yupo, nimezungumza naye asubuhi, angekuwa mgonjwa ningezungumza naye kwa simu?" alihoji.

Baadhi ya vyombo vya habari vya kimataifa vimeripoti uvumi huo, vikimtumia Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, kama chanzo cha taarifa hizo.

Lissu, aliyechuana na Rais Magufuli kuwania kiti cha urais katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka jana kisha kurejea Ubelgiji baada ya matokeo kutangazwa, alinukuliwa na vyombo hivyo akidai kupewa taarifa na vyanzo vyake kuhusu kuugua kwa mpinzani wake huyo wa kisiasa.

Mbunge huyo wa zamani wa Singida Mashariki, anadai kutoonekana kwa Rais Magufuli katika shughuli za kitaifa kwa takriban wiki mbili sasa kunahusiana na hicho anachodai kiongozi huyo wa nchi kutokuwa vizuri kiafya.

Rais Magufuli amekuwa akikosolewa na wapinzani wake kutokana na msimamo wake katika masuala kadhaa ikiwamo kukataa kuwaweka wananchi karantini, kutilia shaka vipimo vya corona na hivi karibuni kutangaza Tanzania kutoipokea chanjo ya corona hadi pale wataalamu wa ndani watakapojiridhisha kuhusu usalama wake.

Katika uongozi wake, Rais Magufuli amepata umaarufu mkubwa duniani kutokana na kufanya mapinduzi makubwa kiuchumi, akitekeleza miradi mikubwa, kuimarisha nidhamu ya utumishi pamoja na kudhibiti rushwa, ufisadi na wizi wa maliasili za nchi.

Ndani ya kipindi cha miaka mitano ya uongozi wake, Rais Magufuli pia amefanikiwa kwa kiwango kikubwa kupunguza matukio ya ujambazi, ujangili na biashara haramu ya dawa za kulevya.

# Zuio la Kenya lilivyoumiza wafanyabiashara mahindi

**Na Waandishi Wetu**

WAFANYABIASHARA wa mahindi mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro, wamebainisha masikitiko yao kuhusu uamuzi wa Kenya kuzuia mahindi ya Tanzania kuingia nchini mwake, wakisema umesababisha athari za kiuchumi kwao kutokana na kushindwa kurejesha mikopo waliyochukua katika taasisi za fedha.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Godfrey Mongi, alisema si kweli kwamba mahindi yanayotoka Tanzania, yana kitu kinachoitwa Aphotexin (uvundo).

Mongi alisema: "Hii ni migogoro ya kibiashara na kimsingi inatuathiri sana sisi wafanyabiashara wa mahindi, wengi tumekopa benki ili kufanya kazi hii ya kutafuta riziki na kujiongezea kipato.

"Hivi sasa ni kama tumeongezewa mzigo na hasara inatunyemelea hasa tunaokodisha malori kusafirisha mahindi kwenda ng'ambo."

Mfanyabiashara John Saibulu alisema kwa sasa hata mwingiliano wa kibiashara kwa wakazi wa mpakani umekuwa hafifu kutokana na raia wa Kenya kutonunua mahindi kwenye stoo zao.

"Athari ipo kwa wafanyabiashara wakubwa na sisi pia wadogo wenye maduka ya vyakula ikiwamo mahindi, hawafiki kununua. Hii ni kutokana na kauli ya serikali yao ya Kenya," alisema.

**ALIA MALORI KUZUIWA**

Wakati Arusha wakilia na hali hiyo, wafanyabiashara wa mahindi mkoani Manyara wameiomba serikali kutafuta ufumbuzi wa suala hilo, wakibainisha zuio hilo lina madhara kwa wafanyabiashara wanaosafirisha mahindi kwenda nje ya nchi.

Mfanyabiashara Clement Fissoo wa Katesh, alisema ni mwathirika wa zuio hilo kutokana na malori yake matano yanashikiliwa tangu Machi 7, mwaka huu huko Kenya.

Alisema malori yake yanayoshikiliwa upande wa Kenya, yana magunia 300 ya mahindi na wanaendelea kufanya mawasiliano kujua kinachoendelea.

Fissoo aliishauri serikali kutafuta ufumbuzi juu ya zuio hilo kwa kuwa wafanyabiashara wa mazao ya chakula hasa mahindi, wanaitegemea Kenya.

Joseph Mushi, mfanyabiashara wa nafaka katika Manispaa ya Moshi, alisema bei ya nafaka imeanza kushuka kutokana na wafanyabiashara wengi kukosa mahali pa kuuza mazao yao baada ya kutangazwa kwa zuio hilo.

"Kwa ujumla, bei imeshuka kutoka Sh. 700 kwa kilo moja ya mahindi hadi 380, jambo ambalo ni hatari, maana bei hii haitulii, kesho unaweza kukuta imeshuka zaidi," alisema.

Mwanzoni mwa wiki, Waziri wa Kilimo, Profesa Adolf Mkenda, alisema suala hilo linashughulikiwa na wizara tatu, ikiwamo anayoiongoza.

Kwa mujibu wa waziri huyo, wizara zingine zinazoshughulikia suala hilo ni Wizara ya Viwanda, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

**●IMEANDIKWA NA HAMIDA KAMCHALLA (TANGA), ZANURA MOLLEL (LONGIDO), JALIWASON JASSON (BABATI) NA GODFREY MUSHI (ARUSHA).**

HABARI KITAIFA

# Radi yaua wanafunzi familia moja

**Na Jumbe Ismailly,** IKUNGI

WANAFUNZI wawili wa Shule ya Msingi Siuyu, Ikungi mkoani Singida, wamekufa kwa kupigwa na radi nyumbani kwao muda mfupi tu baada ya kurudi kutoka shuleni.

Akithibitisha kutokea kwa vifo hivyo, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Siuyu, Bakari Kaduguda, alisema tukio hilo lilitokea Machi 8, saa 9:00 mchana katika kijiji hicho.

Kaduguda aliwataja wanafunzi hao kuwa ni Daudi Muna (13) mwanafunzi wa darasa la tatu na Joseph Leghenjaa (7) mwanafunzi wa darasa la awali katika shule hiyo.

Kwa mujibu wa Kaduguda, siku ya tukio wakati wanafunzi hao wakitoka shuleni, mvua ilianza kunyesha na ndipo walianza kukimbia kuwahi ili wasije kunyeshewa na walipofika nyumbani kwao waliingia ndani na kuanza kuvua nguo za shule.

Alisema wakati Daudi akiendelea kuvua nguo, ndipo mdogo wake James alitoka chumbani na kusimama mlangoni wakati huo mvua ikiwa bado inanyesha.

Kaduguda alisema wakati James anayesoma darasa la awali akiwa amesimama mlangoni, ndipo Daudi naye alitoka chumbani na kumfuata mdogo wake mlangoni na kusimama nyuma yake na ndipo ghafla radi iliwapiga wote wawili na kuanguka chini.

Alisema baada ya wanafunzi hao kudondoka chini ndipo jitihada za kutafuta usafiri wa kuwapeleka Hospitali ya Misheni ya Makiungu zilianza na baada ya kuanza safari ya kwenda kupatiwa huduma, wakiwa njiani, Daudi alipoteza maisha.

Pia alisema walipofika hospitalini wakati wataalamu wakihangaikia kuokoa maisha ya James, naye alifariki dunia.

# Ofisa ardhi mbaroni madai ya kujipatia milioni 95.5/-

**Na Said Hamdani,** LINDI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Lindi, inawashikilia kwa mahojiano watu watatu, akiwamo mtumishi wa Halmashauri ya Mtama kwa kujipatia zaidi ya Sh. milioni 95.5 kinyume cha sheria.

Mbali na mtumishi huyo, pia yumo mjumbe wa serikali ya kijiji ambao wote kwa pamoja wanatuhumiwa kujipatia Sh. 92,562,449.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Lindi, Mhandisi Abtery Mganga, aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Mpima Ardhi Halmashauri ya Mtama, Abdallah Mbinga, Mohamed Mtungwe ambaye ni mjumbe wa serikali ya kijiji cha Nahukahuka 'B' na Hassan Mohamed, mkulima wa kijiji hicho.

Mganga alisema watuhumiwa hao wamejipatia kiasi hicho cha fedha kutoka kwa mwekezaji wa kampuni ya Cassava Starch of Tanzania Limitedi, ikiwa ni malipo ya fidia kwa wakulima wa kijiji cha Nahukahuka 'B' kupisha mradi wa ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza wanga unaotokana na mhogo.

"Huyu mwekezaji alitoa fidia ya jumla ya Sh. 450,336,500 lakini hazikuwafikia walengwa, badala yake waligawana," alisema Mganga.

Alisema baada ya mwekezaji kutoa fedha hizo, Mbinga ambaye ni mpima ardhi katika Halmashauri ya Mtama, anadaiwa kubadilisha taarifa ya uthamini wa mali za wananchi kwa kuondoa jina la kijiji cha Nahukahuka "B" kwenye orodha ya malipo na kuingiza majina matatu likiwemo lake na kusababisha Sh. 80,956,800 zilizostahili kulipwa kijiji husika na badala yake zilikwenda mifukoni mwao.

Mganga alisema kutokana na udanganyifu wa kutumia nyaraka, Mbinga alijipatia Sh. 60,747, 579, Mtungwe Sh. 10,047,645/79 na Mohamed alipata Sh. 21,767,225.

Kutokana na kitendo hicho, alisema watuhumiwa wote kwa pamoja wanakabiliwa na tuhuma tano zikiwamo kutumia nyaraka za uongo, kula njama na kutenda kosa, kughushi nyaraka kwa lengo la kudanganya, kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu na kuisababishia serikali hasara.

Mganga alisema watuhumiwa wote kwa pamoja watafikishwa mahakamani muda wowote kuanzia sasa kujibu tuhuma zinazowakabiri kwa kuwa taratibu zote za kisheria zimeshakamilishwa.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimsikiliza Mwenyekiti wa Bodi ya Chama cha Wawekezaji wa Utalii Zanzibar (ZATI), Seif Masoud Miskry, wakati wa mkutano na wawekezaji wa sekta ya utalii Zanzibar Ikulu jana, ikiwa ni mwendelezo wa mikutano yake kuzungumza na wafanyabiashara wa sekta mbalimbali. **PICHA: IKULU**

# Wanafunzi wasomea chini ya michikichi

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WANAFUNZI wa awali, darasa la kwanza na la pili katika Shule ya Msingi Samilo, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma wanalazimika kusomea chini ya miti ya michikichi kutokana na upungufu wa vyumba vya madarasa.

Kutokana na adha hiyo, wazazi na wanafunzi hao walisema jana kuwa wanaomba serikali itoe msaada wa haraka.

Shule hiyo ina wanafunzi 597 wanaosoma kwenye vyumba vinne vya madarasa na kipindi cha mvua, wamekuwa wakilazimika kusitisha masomo.

Idrisa Ntahundi, mwanafunzi wa darasa la sita katika shule hiyo, alisema kuna wakati mvua inaponyesha wanachanganywa darasa la nne, la tano, la sita na wanafunzi wa shule ya awali.

"Ombi letu watusaidie kuongeza madarasa na madawati. Unakuta tunachanganywa darasa la tano, la sita na awali mlemle hadi walimu wanashindwa kufundisha," alisema.

Mkazi wa Kata ya Mahembe, Seleman Issa, alisema wamekuwa wakijitahidi kushiriki kuboresha mazingira ya elimu na kuomba serikali kuongeza nguvu zaidi ili wanafunzi hao waondokane na adha hiyo.

Diwani wa Mahembe, Mamisho Ruyange, alisema katika kata hiyo, kuna upungufu wa miundombinu ya elimu katika shule tatu za Samilo, Kabanga na Bugumba ambazo zote kuna wanafunzi wanaosomea chini ya miti wakiwa wamekalia matofali.

Alisema tayari aliliwasilisha jambo hilo katika kikao cha baraza la madiwani na wameomba fedha za uboreshaji wa miundombinu kutoka serikali kuu katika bajeti ya mwaka 2020/21.

"Ninaamini serikali yetu itatupatia mgawo ili kuokoa jahazi kwa kuwa wanafunzi wana pata adha sana.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, Pendo Mangali, alisema serikali inatambua upungufu huo na imeshachukua hatua kwa kuomba fedha kutoka serikali kuu.

Pia alisema halmashauri hiyo kwa kutumia fedha za ndani, hutengeneza madawati wanayoyagawa kwenye shule zenye uhitaji.

## TABOA yaibua mapya kuhusu tiketi mtandao

**Na Richard Makore,** MWANZA

CHAMA cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA) mkoani Mwanza, kimemwomba Rais John Magufuli kuingilia kati na kuvunja utaratibu wa kuweka wakala wa kukusanya mapato kwenye ukataji wa tiketi za mtandao badala yake wapatiwe mashine za kielectronic (EFD).

Wamemwomba Rais Magufuli kuvunja utaratibu huo na kutaka wapewe mashine hizo ili kulipa kodi halali za serikali moja kwa moja kwa Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) kama ilivyo kwa wafanyabiashara wengine.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Katibu wa TABOA Mkoa wa Mwanza, Anwar Said, alipozungumza na Nipashe na kusema utaratibu wa sasa utawasababishia washindwe kufanya biashara.

Alisema ngazi zote za chini zimeshindwa kusikiliza na kumaliza tatizo lao na kwamba Rais Magufuli pekee ndiye mwenye uwezo wa kuwanusuru na janga hilo.

Saidi alisema Mamlaka ya Uthibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), imeshindwa kuweka mfumo rafiki wa kuwawezesha kufanya biashara wenyewe bila kupitia kwa wakala wa kukata tiketi na kupata faida ili waweze kulipa kodi halali za serikali.

Alisema wafanyabiashara wengine nchini wanatumia mashine za EFD lakini kwa upande wa wasafirishaji wa abiria kumekuwa na ukandamizaji, hivyo kusababisha baadhi ya wamiliki wa mabasi kushindwa kumudu gharama za uendeshaji.

Walilaumu LATRA kwa kutaka kuingilia mfumo mzima wa ufanyaji biashara ikiwamo kutaka kuwapigia mahesabu ili kujua wanaingiza kiasi gani badala ya kazi hiyo kufanywa na TRA ambao ndiyo waliopewa jukumu la kukusanya kodi.

Aliongeza kuwa kabla ya kuanzisha mfumo wa ukataji wa tiketi mtandao wangeanza kufanyia majaribio ili kuona kama unafaidisha pande zote mbili, yaani serikali na wamiliki wa mabasi.

Katibu huyo alifafanua kuwa mfumo wa tiketi mtandao unasababisha fedha za wafanyabiashara wa mabasi kukusanywa na wakala ambaye hawamjui na kisha yeye azipeleke benki. Baada ya mapato kukusanywa na kupelekwa benki, alisema mfanyabiashara analazimika kwenda kuulizia kiasi kilichoingizwa jambo ambalo wanaona ni ngumu na mara kadhaa utaratibu huo umesababisha fedha zao kupotea.

Naye Mjumbe wa TABOA Mkoa wa Mwanza, Fidel Shiratu, alisema mfumo wa tiketi mtandao hautekelezeki kwa kuwa siyo rafiki kwa wamiliki wa mabasi.

Alisema mfumo huo unamtaka mmiliki kuweka fedha katika mashine yaani 'Flot' na kwamba njia rahisi kwa serikali kukusanya mapato yake ni kuwaruhusu watumie mashine za EFD badala ya kutumia mawakala kama ilivyo sasa.

Shiratu pia alisema matumizi ya vidhibiti mwendo katika mabasi yao 'ving'amuzi' vinawagharimu fedha nyingi kwa mwaka.

Alisema wakiwa wadau, mpaka sasa hawajui mmiliki wa ving'amuzi hivyo na kwamba kwa mwaka wanavilipia zaidi ya Sh. milioni 12 fedha ambazo alisema ni nyingi.

# Manispaa yachangamkia fursa ujio SGR

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

HALMASHAURI ya Manispaa ya Morogoro, imetenga Sh. milioni 500 kwa ajili ya kujenga stendi ya kisasa ya daladala katika eneo inalopita reli ya kisasa (SGR) Kata ya Kihonda ili kuhudumia abiria na wananchi watakaotumia usafiri wa treni hiyo kati ya Morogoro na Dar es Salaam .

Akitoa taarifa fupi ya mipango ya manispaa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22, Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Sheila Lukuba, alisema bajeti hiyo ya awali imelenga kujenga kituo hicho ili kuwapunguzia adha wasafiri watakaotumia treni hiyo.

"Lengo letu ni kuboresha mji wa Morogoro ikiwa ni sambamba na kujenga kituo cha daladala eneo la Kihonda inakopita SGR na awamu ya kwanza tumetenga Sh. milioni 500," alisema Lukuba.

Pamoja na kujengwa kwa stendi hiyo ya kisasa, Lukuba alisema katika bajeti ya mwaka 2021/22, zimetengwa Sh. milioni 180 kwa awamu ya kwanza kwa ajili ya ujenzi wa machinjio ya kisasa yatakayojengwa eneo la Mkundi. "Tunakusudia kuyaondoa machinjio ya sasa ambayo yapo katikati ya mji ambayo yamekuwa kero kwa wananchi kutokana na miundombinu yake kuwa chakavu na tunakusudia kuyajenga eneo la Mkundi na awamu ya kwanza tumetenga Sh. milioni 180," alisema.

Mkurugenzi huyo pia alisema ujenzi huo umepangwa kuanza katika bajeti ya mwaka huo ambao itaanza Julai Mosi, mwaka huu. Katika hatua nyingine, Lukuba alisema kutokana na manispaa kuwa katika kundi A la mpangilio wa manispaa kitaifa zenye kukusanya mapato ya ndani kuanzia Sh. bilioni tano hadi 12, kwa sasa inapaswa kujenga kituo kimoja cha afya kilichokamilika pamoja na madarasa yasiyopungua 40.

Kutokana na masharti hayo, alisema manispaa imetenga Sh. milioni 400 kwa ajili ya kujenga kituo hicho eneo la Kihonda Kilimanjaro ambako kuna eneo na pia kuridhiwa na baraza la madiwani.

Mbunge wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood, licha ya kusifu mpango wa kuwa na vitega uchumi, aliutahadharisha uongozi wa manispaa hiyo kuhakikisha ardhi katika eneo itakapojengwa stendi ya daladala Kihonda -SGR , isiwe na mgogoro na taasisi nyingine.



Walezi wa kituo cha kulelea watoto yatima cha Nuru, jijini Mbeya, wakiwa wamewapakata watoto mapacha wenye umri wa mwezi mmoja ambao mama yao alifariki akijifungua huku ndugu wa marehemu wakigoma kulea watoto hao na kituo hicho kuamua kuwalea mapema wiki hii. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wahukumiwa faini mil. 50/- au jela

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imewahukumu watu wanne akiwamo mfanyabiashara Mohamed Hashimu, kulipa fidia ya Sh. Milioni 50, faini Sh.milioni nne au kwenda jela miaka minne.

Watu hao wamehukumiwa baada ya kupatikana na hatia ya kukutwa na madini yenye thamani ya Sh. milioni 42.9 bila kuwa na kibali cha Kamishna wa Madini.

Kadhalika, mahakama hiyo iliyoketi jana chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi, Godfrey Isaya, iliamuru madini na vielelezo vyote waliyokutwa navyo washtakiwa kutaifishwa kuwa mali ya serikali.

Mbali na Hashim, washtakiwa wengine ni Mohamed Muwas(26), Mohamed Yoonus (28) wote raia wa Sri Lanka na Mtanzania Mehboob Rattansi (62) mkazi wa Msasani.

Hakimu alisema kwa kuwa washtakiwa wamekiri makosa yao baada ya kufanya makubaliano na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), mahakama imewaona wana hatia.

"Washtakiwa wote mtalipa fidia ya Sh. milioni 50, mtalipa faini ya Sh.milioni Moja kila mmoja, mkishindwa mtakwenda jela mwaka mmoja kila mmoja, mahakama yangu inaamuru pia kutaifishwa madini yenye thamani ya Sh. Milioni 42.9, simu za mkononi, kompyuta na vifaa vya kupimia madini kuwa mali ya serikali" alisema Hakimu Isaya. Awali, Wakili wa Serikali Mkuu, Marterus Marandu, akisaidiana na Makili wa Serikali Waandamizi, Wankyo Simon na Ladalaus Komanya, alidai kuwa shauri hilo lilipangwa kwa ajili ya washtakiwa kusomewa maelezo ya awali, baada ya kufanya makubaliano na DPP ikiwamo kukiri makosa hayo.

Mapema mahakamani hapo, washtakiwa walikuwa wanakabiliwa na mashtaka sita, lakini baada ya kufanya majadiliano na DPP, mengine yameondolewa na kukabiliwa na shtaka moja.

Akisoma mashtaka yao, Wankyo alidai washtakiwa kwa pamoja walitenda kosa hilo Januari 8, mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Alidai kuwa siku na eneo hilo, washtakiwa kwa pamoja walikutwa wakimiliki aina 43 za vito vya madini ghafi, yakiwamo ya rubi na tanzanite yenye uzito wa gramu 2,054.4 yakiwa na thamani ya Sh. 25,788,353 bila kuwa na kibali kutoka kwa Kamishna wa madini. Pia walikutwa na madini yaliyoongezewa thamani yenye uzito wa carat 85.89 yakiwa na thamani ya Sh 17,132,702 bila kibali.

Vile vile washtakiwa wanadaiwa kununua madini hayo yenye thamani ya Sh. milioni 42.9 bila kuwa na kibali kutoka mamlaka husika.

HABARI KITAIFA

# Nyumba wadaiwa sugu pango ardhi hatarini kuuzwa

**Na Rose Jacob,** MWANZA

ZAIDI ya wadaiwa sugu 700 wa kodi ya pango la ardhi katika wilaya nne za Mkoa wa Mwanza, wapo hatarini kuuziwa nyumba zao iwapo watashindwa kulipa kodi ndani ya siku 14.

Wamiliki hao walifikishwa jana katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Mwanza, mbele ya Mwenyekiti Magambo Mayeye, wakidaiwa Sh. bilioni 3.3.

Baraza hilo lilikaa jana jijini Mwanza katika uwanja wa Nyamagana na kusikiliza wadaiwa hao ambao wameshindwa kulipa kodi ya pango kwa mujibu wa sheria.

Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Mwanza, Elia Kamihanda, alisema wameamua kuwafikisha katika baraza wadaiwa sugu 736 baada ya kushindwa kulipa kodi.

"Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi kama mmiliki atapokea hati ya kumtaka kulipia deni lake ndani ya siku 14 na akashindwa, Kamishina wa Ardhi amepewa haki ya kumfikisha mahakamani mdaiwa ndani ya siku hizo. Katika hao wako wadaiwa wa miaka miwili na kuendelea," alisema Kamihanda.

Alisema wadaiwa hao wanatoka katika wilaya za Nyamagana, Misungwi, Magu na Ilemela mkoani Mwanza.

Aliongeza kuwa kesi zilizoko ni 1,000 ambazo wadaiwa wanadaiwa jumla ya Sh. Bilioni 12 na kwamba kati ya hizo, kesi 736 ndizo zimefikishwa mahakamani kwa awamu ya kwanza.

Kifungu cha 50 cha Sheria ya Ardhi, kinasema mmiliki akipewa hati ya madai ndani ya siku 14, ofisi ya kamishina ina jukumu la kumfikisha mahakamani ili ofisi ya ardhi ipewe kibali cha kukamata mali na kumfutia hati mdaiwa ili apewe mtu mwingine.

Baadhi ya wananchi walioitwa katika uwanja huo wa Nyamagana walisema, wamepewa siku 14 wawe wamelipa malimbikizo ya madeni yao.

Walisema baadhi wameomba kulipa kidogo kidogo, lakini waliambiwa wahakikishe wanamaliza deni lote ndani ya siku 14, vinginevyo mali zao ambazo ni nyumba zitauzwa kwa mnada.



Wasamaria wema wakisaidia kulisukuma gari lililozimika katikati ya barabara ya Morogoro, eneo la Ubungo, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Shule za wasichana kidato cha tano sasa kujengwa kila mkoa

**Na Augusta Njoji,** MOSHI

SERIKALI imejipanga kujenga shule 26 za wasichana kila mkoa kwa ajili wanafunzi watakaofaulu kuingia kidato cha tano na sita ili kusoma bila kikwazo na kufikia ndoto zao.

Ujenzi wa shule hiyo utafanywa kupitia Mradi wa maboresho ya Elimu ya Sekondari (SEQUIP), ambao umetokana na matunda ya utekelezaji mzuri wa Mradi wa Lipa kulingana na Matokeo (EP4R).

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Gerald Mweli, alisema mradi SEQUIP utatekelezwa kwa miaka mitano (2020/21 - 2025/26) na unatokana na mkopo kutoka Benki ya Dunia.

"Chini ya EP4R tumefanya kazi kubwa kuhakikisha mtoto wa kike anapata nafasi yenye usawa. Watoto wa kike walioingia kidato cha kwanza mwaka huu ni zaidi ya 430,000. Hata takwimu zingine zote za kuingia darasa la kwanza, kidato cha tano wanaongoza watoto wa kike," alisema.

Mweli alisema kutokana na watoto wa kike kuongezeka kwenye ufaulu, serikali itahakikisha watoto wote wa kike wanaofaulu wanaingia kidato cha tano.

"Lengo kuongeza watoto 13,000 wanaofaulu waingie kidato cha tano ifikapo mwaka 2025. Malengo hayo nadhani tutafikia kabla ya hapo tumeshajipanga kama serikali, ifikapo mwaka 2023 malengo ya SEQUIP yawe yametekelezwa," alisema.

Pamoja na ujenzi wa shule hizo, alisema mradi huo ambao Benki ya Dunia imeidhinisha mkopo wa Dola za Marekani milioni 500 sawa na Sh. trilioni 1.2, pia utajenga shule zingine mpya 1,000 za kutwa zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 400 kwa kila shule.

Naye, Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Weruweru, Rosalia Frimi, alisema kujengwa kwa shule nyingi za wasichana kutasaidia kupunguza tatizo la mimba kwa wanafunzi.

"Kwa mfano katika shule hii ya wasichana tunawafundisha mambo mbalimbali mbali na masomo ikiwamo namna ya kujitunza, kuepuka vishawishi, kwa kweli tunasimamia nidhamu ya mtoto wa kike ili kujenga kuwa kiongozi, msomi na mama," alisema.

# Maambuziki VVU Songwe yazidi kushuka

**Na Thobias Mwanakatwe**

SERIKALI mkoani Songwe imetangaza kushuka kwa kiwango cha maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi (VVU) kutoka asilimia 5.8 kwa mwaka 2017 hadi asilimia 3.48 mwaka huu.

Songwe ni mkoa mpya ambao ulimegwa kutoka Mkoa wa Mbeya na hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema watagawana takwimu za maambukizi ya VVU ambayo yapo kiwango cha asilimia 9 kama walivyogawana mali na vitu vingine wakati wanaugawa mkoa wa huo.

Hata hivyo, kabla ya kufanyika kwa kikao hicho, serikali mkoani Songwe imetangaza kushuka kwa kiwango cha maambukizi hayo.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nicodemus Mwangela, alisema hayo juzi wakati akitoa taarifa juu ya mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI kwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, aliyekuwa kwenye ziara ya siku moja mkoani humo.

Jenerali Mwangela alisema matokeo hayo ya kushuka kwa kiwango cha maambukizi mapya ya UKIMWI ni jitihada za pamoja za wadau dhidi ya mapambano ya VVU mkoani Songwe.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2020/21, Sh. 2,229,381,503 sawa na asilimia 12 zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza afua za kupambana na virusi vya UKIMWI kutoka serikalini pamoja na wadau wengine.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Dk. Hamad Nyembea, akitoa takwimu za hali ya maambukizi, alisema mkoa una takribani watu 43, 819 wanaoishi na VVU na kwamba asilimia 99 ya watu wote waliobainika kuambukizwa VVU wako katika tiba na matunzo, huku asilimia 94 wana ufubavu wa VVU.

Dk. Nyembea alisema mkoa huo una vituo 68 vinavyotoa huduma za mafunzo na tiba (CTC) na vituo 172 vinatoa huduma za kuzuia maambukizi.

Dk. Gwajima alipongeza jitihada hizo za serikali ya Mkoa katika vita dhidi ya UKIMWI.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ushindani Ligi Kuu Bara unadhihirisha mapinduzi

**WAKATI** Ligi Kuu Bara inatarajia kukamilisha mzunguko wa 24 leo, ushindani umeendelea kuonekana na kuongezeka katika mechi za ligi hiyo inayoshirikisha timu 18 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.

Ligi Kuu Bara ndio hutoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo hufanyika kila mwaka kwa kusimamiwa na kuandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF). Ushindani huo umeongezeka zaidi msimu huu baada ya kuwapo kwa dalili za Tanzania Bara kuwakilishwa na timu nne kwenye mashindano ya kimataifa ya CAF katika msimu ujao baada ya Simba kufanya vizuri kwenye michuano hiyo inayoendelea hivi sasa. Simba, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao wametinga katika hatua ya makundi, wameiongezea nchi pointi na hivyo kutarajiwa kupata nafasi ya kutoa timu mbili kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na nyingine mbili katika mashindano ya Kombe la Shirikisho.

Tofauti na misimu mingine iliyopita ambapo timu zinazoshiriki hujigawa katika makundi mawili ambayo la kwanza ni lile la vigogo wanaopigana vikumbo kuwania taji la ubingwa na lingine ni la wale wanaopambana kujinusuru na janga la kushuka daraja.

Hapa sura ilionekana wazi kwa sababu walioko chini walikuwa wanapambana kuhakikisha wanarekebisha upungufu wao wa mzunguko wa kwanza kwa kusaka ushindi na kujiweka katika nafasi salama huku wale waliocheza karata zao vizuri mwanzoni, waliendelea kujiimarisha ili kutimiza malengo yao.

Msimu huu mbali na kuwania ubingwa, zipo klabu ambazo zinapambana kuhakikisha zinamaliza msimu katika nafasi nne za juu kwa ajili ya kujiweka kwenye mazingira ya kupata nafasi ya kuiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya CAF kama hesabu zitakwenda sawa sawa na matarajio ya wengi.

Kwa maana hiyo, mpaka sasa bado hakuna timu ambayo ina nafasi ya asilimia 100 katika kutimiza malengo yake kwa sababu idadi ya michezo iliyobakia ni kubwa na lolote huweza kutokea katika mchezo huo wa soka.


Nipashe inazikumbusha timu zinazowania taji kuendelea kuongeza umakini kwa sababu bado njia ni nyeupe na hata timu ambayo iko nje ya 'Tano Bora' kwa sasa inaweza kufanya vyema na hatimaye kutawazwa mabingwa wapya wa msimu wa 2020/21.

Vile vile inazitaka timu ambazo zinaburuza mkia kutokata tamaa kwa sababu bado safari haijamalizika na umakini, weledi na kuheshimu wapinzani wote kutawasaidia kuwanusuru na jinamizi la kushuka daraja ambalo linawazunguka.

Imekuwa ni kama desturi kwa baadhi ya timu kukamia au kucheza katika kiwango bora pale tu wanapokutana na Simba au Yanga na timu hiyo kucheza bila mipango inapokutana na klabu nyingine, na matokeo yake hupata matokeo mabaya kwenye michezo hiyo ambapo kimsingi yote ina hadhi sawa. Tunakumbusha viongozi, makocha na wadau kufanya maandalizi yanayofanana katika kila mchezo kwa ajili ya kujiweka katika nafasi salama kuanzia mwanzo wa msimu, na kuacha tabia ya kuongeza nguvu pale tu wanapokaribia kukutana na vigogo hao wa soka nchini. Kwa upande wa wachezaji, tunawakumbusha kucheza katika kiwango cha juu kwenye michezo yote ili kujiuza kwa mawakala na makocha wa timu za taifa, ambao hufuatilia mechi mbalimbali kwa lengo la kusaka vipaji, kuviita ili kulitumikia taifa.

Lakini kwa upande mwingine, ushindani ambao unaonekana katika mechi zinazoendelea, unamaanisha hakuna timu ambayo inaingia uwanjani ikiwa na matokeo yake mfukoni, kila timu inatakiwa kupambana kusaka matokeo mazuri ndani ya dakika 90 rasmi na kutotegemea fitna za nje ya uwanja. Kufanya vizuri kwa Ligi Kuu Tanzania Bara, ni ishara njema kwa kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), kuwa imara kwa sababu nyota wake wengi huitwa kutoka katika hiyo ambao huungana na wachezaji wanaosakata kandanda kwenye mataifa ya ughaibuni wakiongozwa na nahodha, Mbwana Samatta.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Leo kwako kesho kwa mwenzio

**JAMBO** linalokupata leo liwe la shida au raha huweza kumpata mwenzio kesho.

Methali hii hutumiwa kutunasihi tusiwacheke wenzetu wanaokumbwa na matatizo kwa kuwa yanaweza kutukumba sisi pia. Huweza kutumiwa kumtanabaisha mtu anayejitapa kwa kuwa na hali nzuri kuwa kesho huenda asiwe na hali hiyo na badala yake awe nayo mwenzake aliyemdharau.

Yanga na Simba ndizo timu maarufu nchini Tanzania na zinazojulikana zaidi nje ya nchi. Sababu ni kwamba ndizo zilizoanzishwa zamani zaidi, zenye nguvu kuliko zote nchini na zenye wanachama na mashabiki wengi zaidi.

Ni vilabu vinavyopapatikiwa na watu wanaotaka wajulikane zaidi nchini kwa sababu wazijuazo na wengine kutaka kujinufaisha kwa fedha za vilabu hivyo kongwe kwa kile kiitwacho "kupiga pesa!" Angalau wanaogombea uongozi ili wafahamike zaidi wanaweza kufanya mambo mengi ya maendeleo kwa vilabu vyao lakini sio wale wanaogombea nafasi mbalimbali za uongozi ili wajinufaishe kupitia fedha za timu hizo, na hasa zinazotolewa na wafadhili.

Hata hivyo wanagonga mwamba kwa wafadhili ambao husimamia utoaji wa fedha zao hasa katika usajili wa wachezaji, mishahara yao, walimu na mambo mengine yanayohusu maendeleo ya klabu. Hivi karibuni mashabiki wa Yanga na Simba walichekana sana timu zao zilipotoka sare dakika za mwisho kwenye michezo yao ya ligi. Yanga ilikuwa ikiongoza kwa bao 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania lakini furaha yao iligeuka huzuni baada ya Maafande hao kusawazisha dakika chache kabla ya mwisho wa mchezo na kufanya mchezo umalizike kwa sare ya bao 1-1. Mashabiki wa Simba waliwacheka sana wenzao wa Yanga kwa sare ile.

Siku iliyofuata ilikuwa zamu ya Simba kupambana na timu ya Magereza kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. Prisons iliyokuwa mbabe kwa bao 1-0 dhidi ya Simba ilishangiliwa sana na mashabiki wa Yanga wakijua Simba imepoteza mchezo huo lakini ilisawazisha zikiwa zimebaki dakika tano kuwa mwisho wa mchezo!

Mashabiki wa Simba walishangilia kwa nderemo na kuwaacha wenzao wa Yanga kwenye bumbuazi!

Timu hizi mbili (Yanga na Simba) kuitwa watani wa jadi sipingi hata kidogo kwani ni haki kutaniana na kuchekana mojawapo inaposhindwa na timu yoyote ya Tanzania. Nisichokubaliana na mashabiki wa pande zote mbili ni upumbavu wao wa kushirikiana na timu za nje ya Tanzania zinapozifunga Yanga au Simba!

Huo si utani wa jadi bali ni ujinga wa mashabiki wa timu za Yanga na Simba kutojua maana ya udugu, yaani uhusiano wa watu wanaotokana na uzawa mmoja. Hapa nazungumzia Utanzania wetu. Mashabiki wa pande zote mbili wanapozishangilia timu ngeni kutoka nje ya Tanzania wanaonyesha ujinga wao kwa wageni!

Wahenga walisema: "Habari ya nyumbani simfunulie jirani," maana yake sio vizuri kumfunulia jirani siri za nyumbani. Kwa muktadha huu ni Tanzania na nchi za ughaibuni yaani nchi zilizo n-nje ya nchi yetu.

Wallahi (kwa jina la Mwenyezi Mungu; tamko la kiapo cha kuthibitisha kuwa linalosemwa ni kweli) kama timu za Yanga na Simba zingekuwa zinapambana na timu ngeni kuwa vita vya silaha kisha upande mmoja kuishangilia timu ngeni ilhali bendera ya Tanzania inapepea, hapana shaka timu husika ingeona cha mtema kuni kwa kuisaliti timu ya nyumbani!

Ndo maana hukataa Yanga na Simba kuitwa "watani wa jadi" Ebo! (tamko linaloonyesha hisia ya dharau inayotokana na kukasirika au kutoridhika.) Nduguyo anashambuliwa na mgeni kisha wewe unamshangilia adui anayempiga nguguyo? Pukachaka (neno lenye kuashiria kutema mate ambalo humaanisha kukidharau kitu kilichotajwa.)

Wahenga walisema: " Ndugu mbaya hushinda rafiki mzuri." Maana yake hata kama rafiki atakuwa mzuri kiasi gani hawezi kuwa sawa na ndugu yako hata akiwa mbaya!

Methali hii yaweza kutumiwa kutukumbusha umuhimu wa kuwathamini ndugu zetu au watu tulio na ujamaa nao kwa kuwa wanaweza kutufaa kuliko wanavyoweza kufanya marafiki wageni ambao ni wapita njia. Kama hutaki kuishangilia timu ya nyumbani kama Simba na Namungo zilivyo sasa usiende uwanjani au kama utakwenda kutazama mchezo, acha kuzishangilia timu ngeni. Vinginevyo wewe ni mchawi usiyejua maana ya udugu!

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

## Upatikanaji wa maji wafikia asilimia 73

**Na Happy Severine,** MASWA

WAKALA wa Maji na Usafi na Mazingira Vijijini (RUWASA), Maswa mkoani Simiyu imeongeza upatikanaji wa maji safi na salama vijijini kutoka asilimia 69 hadi asilimia 73.

Hayo yalielezwa jana mjini hapa na Meneja wa RUWASA Wilaya ya Maswa, Boniphace William, wakati wa ziara ya siku mbili ya kutembelea miradi ya maji.

William alisema wilaya hiyo imetekeleza miradi minne ya maji vijijini yenye gharama ya Sh Bilioni 1.3 za lipa kwa matokeo (PFOR) ambazo utekelezaji wake umefanyika katika mradi wa maji wa Isageghe, Masela, Ilamata na Isulilo-Ngongwa hadi Mwamihanza.

Alisema miradi hiyo ya maji iliyojengwa na kukamilika imeongeza upatikanaji wa maji kwa wananchi wa vijijini.

Wananchi wapatao 17,500 kati ya 379,000, wamenufaika na huduma hiyo wilayani Maswa.

Kwa mujibu wa meneja huyo, kitendo cha utekelezaji wa miradi ya maji kupitia 'force akaunti' kimesaidia kutekeleza miradi kwa asilimia 100 kwa gharama ndogo tofauti na kama wangetumia mkandarasi.

Aidha, alisema kuna miradi mingine ya maji inatekelezwa wilayani humo kupitia Mfuko wa Taifa wa Maji katika vijiji vya Nyashimba, Muhida, Nguluguli, Mwamanenge na Sengwa.

William aliongeza kuwa katika miradi hiyo, mradi wa maji wa Sengwa utapata maji kutoka mradi wa Ziwa Victoria toka wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga.

Mkuu wa Wilaya ya Maswa, Aswege Kaminyoge, aliagiza vyanzo vyote vya maji vitunzwe na pia viwe na hati miliki ili kuondoa migogoro ya ardhi ambayo inaweza kujitokeza siku za usoni.

"Natoa maagizo kwa maeneo yote ya miradi ya maji na maeneo mengine yenye taasisi za serikali katika wilaya ya Maswa iwe na hati miliki ya ardhi ili kuondoa migogoro ambayo inaweza kujitokeza kwa siku zijazo," alisema.

Pia alipiga marufuku shughuli zo za kibinadamu katika maeneo ya vyanzo vya maji ili kuvitunza viendelee kuwapatia wananchi maji safi na salama.

# PM kuzindua mwongozo uwekezaji Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa anatarajiwa kufanya ziara ya siku mbili mkoani Mbeya kuanzia kesho na kuzindua miradi mbalimbali ikiwamo mwongozo wa wawekezaji wa mkoa.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema mpango huo unaainisha fursa mbalimbali za uwekezaji katika maeneo yote ya mkoa.

Chalamila alisema mpango huo umefafanua vivutio vya uwekezaji vilivyopo katika kila halmashauri ya mkoa na kwamba ndio utakuwa unatumika kwenye uhamasishaji wa wawekezaji wa ndani na nje. "Waziri Mkuu atatuzindulia mpango huu na kwenye kitabu hiki tumeainisha vivutio vya uwekezaji katika kila halmashauri na tumezingatia vitu mbalimbali kwenye uandaaji wa mwongozo huu ambavyo tunaamini vitatusaidia," alisema Chalamila.

Alisema Waziri Mkuu pia ataweka jiwe la msingi kwenye ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) kinachoendelea kujengwa wilayani Mbarali.

Pia alisema katika ziara hiyo, Waziri Mkuu atazindua jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Wilaya ya Rungwe ya Makandana ambalo limejengwa kwa zaidi ya Sh. milioni 481 na kwamba ujenzi wa jengo hilo ilikuwa ni ahadi ya Rais John Magufuli alipokuwa ziarani wilayani humo.

Baada ya kutoka Rungwe, Waziri Mkuu atakwenda Kyela ambako atazindua ujenzi wa kituo cha pamoja cha forodha kati ya Tanzania na Malawi ambacho kinajengwa katika Mji wa Kasumulu wilayani humo.

Alisema kituo hicho cha forodha kinajengwa kwa awamu tatu na kwamba mpaka kukamilika kwake kitagharimu Sh. bilioni 26 ambazo kati yake Sh. bilioni 13 zitatumika katika awamu ya kwanza.

"Mbeya ni lango la kuingilia katika nchi za ukanda wa SADC (Jumuiya na Maendeleo Kusini mwa Afrika) , hivyo kituo hiki kitatusaidia kuunganisha uchumi wa nchi yetu na wenzetu wa Malawi," alisema.

Chalamila alisema baada ya uzinduzi huo, Waziri Mkuu atatembelea Shule ya Sekondari Kafundo ambayo ni ya mfano katika Mkoa wa Mbeya kwa ujenzi wa mabweni kwa ajili ya wasichana ili kukabiliana na tatizo la mimba kwa wanafunzi.

Katika hatua nyingine, Chalamila aliitaja miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo ilitelekezwa katika mkoa kwa kutumia fedha ambazo zilitolewa na serikali kuu.

Aliitaja baadhi ya miradi hiyo kuwa ni ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya ambalo linajengwa kwa gharama ya Sh. bilioni tisa, ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ambalo linagharimu zaidi ya Sh. milioni tatu.



Wafanyabiashara wa mkaa wakiwa wamepakia bidhaa hiyo kwenye pikipiki katika eneo la Visiga Madafu, mkoani Pwani jana, kwaajili ya kupelekwa sokoni. Wananchi wanatakiwa kuelemishwa kuhusu matumizi ya teknolojia ya nishati mbadala ambayo ni rahisi na yenye uhakika ili kupunguza matumizi ya mkaa yanayosababisha ongeza la matukio ya ukataji wa miti ovyo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# RC ataka ubora ukarabati wa barabara

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, amewaagiza makandarasi wanaokarabati barabara zinazounganisha wilaya za Kongwa, Kiteto, Chemba na Kondoa kuzingatia ubora na viwango na kuzikamilisha kwa wakati.

Makandarasi hao ni anayekarabati barabara ya Kongwa hadi Dosidosi mpakani na Kiteto, Musons Engeneers na Technics Construction Group Limited anayekarabati barabara ya Mrijo hadi Kolo Kondoa na Afritrast Group Limited anayekarabati barabara ya Bicha hadi Mondo, wilayani Chemba.

Dk. Mahenge alitoa maagizo hayo baada ya kukagua barabara hizo na kubainisha kuwa miundombinu hiyo ni muhimu katika usafirishaji wa mazao, hivyo ni lazima zikarabatiwe kwa ubora na viwango vinavyotakiwa.

Alisema ziara hiyo imelenga kukagua utayari wa miundombinu hiyo baada ya mvua kunyesha kisha kuanza kukarabatiwa kwa kuwa barabara ni muhimu hasa kutokana na wilaya hizo kuwa na idadi kubwa ya wakulima.

"Nimekuja kuangalia barabara hizi, tunajua mvua zimenyesha na njia zote tulizopita mazao yamekubali baada ya kipindi cha mvua kuisha mazao yatatakiwa kusafirishwa nimekuja kuona je, barabara zinautayari.

"Tumeona barabara hizi zimeanza kukarabatiwa hivi karibuni tunakumbuka kwenye kikao cha barabara tuliambiwa makandarasi wapo 'site' lakini fedha hamna lakini sasa fedha imetoka nimekuja kuona je, kazi zinaendelea?" alisema. Pia alisema Serikali ina mpango wa kujenga barabara ya lami kutoka Handeni mkoani Tanga- Mrijo- Chemba hadi Singida na kukamilika kwake zitafungua shughuli za kiuchumi katika mikoa hiyo.

Dk. Mahenge aliwataka wananchi kuacha kufanya shughuli zozote kando ya barabara hizo hasa kilimo sambamba na kupitisha mifugo ili zidumu kwa muda mrefu na wananchi kuepukana na madhara yanayotokana na miondombinu ya barabara kuwa mibovu.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADSO) Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Salome Kabunda, alisema barabara zote zinamakandarasi wanaoendelea na ukarabati. Alisema barabara ya njia panda ya Hogolo - Kongwa hadi Dosidosi mpakani na Wilaya ya Kiteto, Manyara, inayokarabatiwa kwa Sh. milioni 580 pia ilijumuisha ukarabati wa daraja la Zoisa ambalo liliharibiwa na mvua na kulikarabati kwa muda kusubiri ujenzi wa daraja jipya.

Pia alisema kipande cha barabara ya Kibaya Wilaya ya Kiteto hadi Mrijo Wilaya ya Chemba nayo tayari ina mkandarasi ambaye bado hajaanza kuikarabati na itaanza kukarabatiwa hivi karibuni.

HABARI KITAIFA

# Kasi ya mimba kwa wanafunzi sasa yapungua

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

TATIZO la mimba kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari katika kata ya Usanda wilayani Shinyanga, zimepungua tofauti na miaka mitatu iliyopita.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Kata ya Usanda, Halima Tendego, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake.

Alisema elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia imesaidia kupunguza mimba za wanafunzi pamoja na ndoa za utotoni katika kata hiyo.

Tendego alisema miaka mitatu iliyopita katika kata hiyo kulikuwa na tatizo la wanafunzi kupewa ujauzito na kuacha masomo, pamoja na wengine kuolewa ndoa za utotoni ambazo zilichangia kuzima ndoto zao. “Mimba za wanafunzi kwenye kata hii zimepungua sana, tofauti na miaka mitatu iliyopita, ambapo awali kwa mwaka mzima wanafunzi 18 walikuwa wanapewa ujauzito na kuacha masomo, lakini kwa sasa inatokea wanafunzi watatu tu,” alisema Tendego.

Naye Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Emmanuel Maduhu, alisema wamekuwa wakiendelea kutoa elimu kwa wananchi kuacha kuwarubuni wanafunzi na kuwaozesha ndoa za utotoni.

Alisema elimu hiyo hutolewa kupitia kwenye mikutano ya hadhara hatua ambayo imesaidia kupunguza mimba hizo za wanafunzi.

Ofisa Elimu Kata ya Usanda, Sospeter Kasonta, alisema elimu ya masuala ya ukatili wa kijinsia imesaidia kupunguza tatizo hilo kwa wanafunzi tofauti na miaka ya nyuma.



Wananchi wakijitolea kuweka kalavati za kupitisha maji katika barabara inayounganisha vijiji vya Madafu na Madabara, Mkoa wa Pwani, mapema wiki hii, kutokana na eneo hilo kuwa korofi hasa nyakati za mvua. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waziri asema elimu mtandao hairidhishi

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, ameiagiza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kutoa elimu ya kutosha kwa umma kuhusu matumizi ya mtandao kutokana na kiwango cha kuelimisha umma kinachotolewa sasa kutokutosheleza.

Dk. Ndugulile alisema hayo juzi alipotembelea ofisi za mamlaka hiyo Zanzibar, akiambatana na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Zanzibar, Rahma Kassim Ali, makatibu wakuu wa wizara, Dk. Zainab Chaula na Amour Bakari.

“TCRA bado sijaridhishwa na kiwango cha elimu ya matumizi ya mtandao mnayoitoa kwa umma na katika utoaji wa elimu kwa umma mkumbuke kuelimisha jamii kuhusu wajibu na haki zao ili wanapopata shida mitandaoni wajue wapite katika njia zipi”, Dk. Ndugulile

Pioa aliielekeza TCRA kuimarisha mfumo wa ukaguzi wa vifaa vya kielektroniki vinavyouzwa na wafanyabiashara ili kuthibitisha ubora na uhalali wa vifaa hivyo ikiwezekana viwekewe alama kuwa vimekaguliwa ili kuhakikisha usalama wa vifaa hivyo kwa matumizi ya wananchi.

Katika hatua nyingine, Dk. Ndugulile aliielekeza TCRA kuhakikisha Shirika la Posta Tanzania linafanya kazi yake ya kusafirisha vipeto na vifurushi kwa kufuata sheria ya EPOCA inayosema kuanzia uzito wa 0 hadi gramu 0.5 haruhusiwi msafirishaji yeyote kusafirisha isipokuwa shirika hilo na kuitaka TCRA kusimamia vyema suala hilo.

Hata hivyo, Dk. Ndugulile alipongeza mamlaka hiyo kwa kupeleka vifaa vya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) katika Shule ya Sekondari ya Wasichani ya Utaani, Wete, kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi na walimu.

Vifaa hivyo ni pamoja na kompyuta 10, printa, projekta pamoja na kuunganisha huduma ya mtandao katika shule toka mwaka 2016 na mpaka sasa bado vipo na vinaendelea kutumika.

Naye Waziri Rahma aliitaka TCRA kuendelea na utaratibu wa kutoa elimu kwa umma juu ya matumizi sahihi ya TEHAMA huku wakijikita zaidi kwenye matumizi ya simu za mkononi.

Mkuu wa TCRA Zanzibar, Esuvatie Masinga, alisema mamlaka inaendelea kujipanga vizuri katika utoaji wa elimu kwa umma na wiki hii tayari wameshatoa mafunzo ya matumizi ya TEHAMA kwa masheha 120 kwa Unguja na Pemba.

# DC awahimiza wafanyabiashara kulipa kodi

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Wilaya ya Temeke (DC), Godwin Gondwe, amewataka wafanyabiashara katika wilaya hiyo kulipa kodi sambamba na kujiwekea utaratibu wa kutunza kumbukumbu za kibiashara ili ziwasaidie wakati changamoto zinapojitokeza.

Gondwe aliyasema hayo jana ofisini kwake na kubainisha kuwa katika wilaya hiyo kuna zaidi ya watu milioni mbili ambao wanaongeza chachu ya ufanyikaji biashara katika eneo hilo.

Pia aliishukuru Serikali kwa jitihada inayoendelea kuzifanya hasa katika suala la ukusanyaji kodi kwa kuwa lina uwiano na miradi inayotekelezwa nchini.

Alisema kutokana na mapato ambayo Serikali inayakusanya, kila mwananchi anaona sehemu mbalimbali nchini ikiwamo Temeke miradi ya kimaendeleo inaendelea kutekelezwa.

“Kutokana na suala hilo, kila mwananchi anafahamu kabisa kuwa anapolipa kodi Serikali inatekeleza mambo yenye manufaa kwa jamii hususani katika elimu, afya na huduma ya maji. Hivyo tukiwa viongozi tunaona uwiano kati ya kodi inayokusanywa na miradi inayoendelea kufanyika,” alisema.

Aliongeza kuwa Serikali imeandaa timu ya wataalamu chini ya Dk, Edwin Mhede, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) watakaoongeza uelewa juu ya ulipaji kodi kwa wananchi wa wilaya ya Temeke.

Gondwe alisema kuna kodi za aina nyingi, hivyo baada ya wataalamu hao kutoa elimu kwa wanaTemeke itawasaidia kujua taratibu za ulipaji wa kila aina ya kodi na aliishukuru TRA kwa kuanza kutekeleza suala hilo ndani ya Wilaya ya Temeke.

Meneja wa TRA Temeke, Paul Walalaze, alisema hawajawasubiri wafanyabiashara wawafuate ofisini ila wameamua kuwafuata katika milango yao ya kibiashara ili kuhakikisha kwamba wanawapatia elimu ya mlipa kodi.

Alisema suala hilo lilianza juzi na litadumu kwa siku 16 ambapo ukomo wake kwa ndani ya wilaya hiyo itakuwa Machi 26.

“Suala hili ndani ya Wilaya ya Temeke limepewa zaidi ya nusu mwezi hivyo tuhakikishe kwamba ndani ya muda uliowekwa elimu inayokusudiwa kutolewa iwafikie wana Temeke wote,” alisema.

Aidha, alibainisha kuwa hiyo ni awamu ya kwanza ya ulipaji kodi na kuna wafanyabiashara wanaolipa kwa awamu na kwa inayoanzia Januari hadi Machi 2021 mwisho itakuwa ni tarehe 31 ya mwezi tajwa.

Alisema suala hilo litajumuisha ukumbushwaji wa namna ya kulipa kodi na uwasilishaji wa makadirio yao katika ofisi za TRA ambazo ndani ya wilaya hiyo ziko kata za Keko, Tazara, Mbagala na Kigamboni.



# Waziri ataka wachimbaji kutumia wataalam wa madini na kuacha ramli

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, amewataka wachimbaji wadogo kutumia Wakala wa Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) katika utafiti badala ya kutegemea ramli.

Aidha Biteko, amewataka wachimbaji hao kubadilika ili wafanye uchimbaji wenye tija na kuleta matokeo chanya kwao na taifa kwa ujumla.

Waziri Biteko aliyasema hayo jana jijini hapa wakati akizindua kitabu cha mwongozo wa namna bora ya uchukuaji sampuli kwa ajili ya uchunguzi wa madini, uliombatana na mafunzo ya wachimbaji wadogo. "Mafunzo hayo ni matokeo ya mkutano wa madini wa kimataifa uliofanyika hivi karibuni jijini Dar es Salaam ambapo mkutano huo ni moja ya maazimio yaliyoafikiwa siku hiyo," alisema.

Biteko alisema GST imekuwa ikifanya kazi na wachimbaji wadogo kwa muda mrefu hivyo imebaini kero ambazo wanakutana nazo na kuamua kuzifanyia kazi kwa vitendo.

Mbali na hilo, Biteko alisema wachimbaji wadogo ili wapige hatua kutoka walipo sasa, wanatakiwa kutumia mbinu za kisayansi kwa ajili ya kuleta tija katika uchimbaji wanaofanya.

Pia alitoa wito kwa watendaji wa Wizara ya Madini na taasisi zake wafanye kila linalowezekana kutoa ushirikiano kwa wachimbaji wadogo. "Wachimbaji wadogo wanatakiwa kujifunza mambo mbalimbali kuhusu madini ili wanapokutana na kero katika uchimbaji wao wajue jinsi ya kukabiliana nayo," alisema Biteko.

Waziri alisema Wizara ya Madini ipo kwa ajili ya kuwahudumia wachimbaji hao wakati wowote watakapowahitaji, kwa kuwa lengo lao ni kukuza na kuendeleza sekta ya madini.

Aidha, aliwataka watendaji wa GST wawafuate wachimbaji katika migodi na machimbo yao na kutoa mafunzo wakiwa katika eneo la kazi.

Mtendaji Mkuu wa GST Dk. Mussa Budeba, alisema mwongozo wa kitabu hicho umeandaliwa kwa ajili ya kumsaidia mchimbaji kujua mahali gani madini yalipo.

"GST ina watalaamu waliobobea ambao watatumia utalaamu waliokuwa nao ili kuwasaidia wachimbaji hao kupata majibu ya uhakika kuhusu wapi kuna madini," alisema Dk. Budeba. Katika kuboresha mwongozo huo, mtendaji mkuu huyo alisema kwa kuanzia, wanatarajia kuzindua Ofisi ya Kanda ya GST Mkoa wa Geita ambayo itakuwa ikiwasaidia wachimbaji hao.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi), Elius Mwakalinga, akizungumza na watumishi wa sekta ya ujenzi katika kikao kazi, jijini Dodoma jana. **PICHA: WUU**

# Wanasiasa wanolewa haki za mtoto Elimu Jumuishi

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

OFISA Mradi wa Elimu Jumuishi Mkoa wa Dodoma, Jane Mgidange, amesema wamejikita zaidi kwenye kuboresha miundombinu shuleni na kuwajengea uwezo wanajamii na wanasiasa ili kutambua haki za mtoto mwenye mahitaji maalumu.

Mgidange alisema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza kwenye mafunzo yaliyowakutanisha viongozi wa taasisi za kiraia zinazojihusisha na ushawishi na utetezi wa elimu jumuishi nchini.

Alisema kazi ya mradi huo ni kuhakikisha watoto wanaosoma katika mazingira jumuishi wanapata vifaa saidizi ambavyo vitawasaidia kupata haki zao za msingi za elimu sawa na watoto wengine wasiokuwa na ulemavu.

Pia alisema mradi huo unahakikisha watoto hao wanasoma kwenye shule na wanapata vifaa vyote vikiwamo vya usaidizi ili wapate mahitaji yao yatakayo wawezesha kuelimishwa sawa na wengine.

Sambamba na hilo, alisema mradi huo pamoja na kusaidia watoto wenye uhitaji maalum, umekuwa ukiwakutanisha na vyombo vya habari ili kufikisha elimu kwa jamii juu ya masuala yanayofanywa na elimu jumuishi.

"Wanahabari ni wadau wakubwa sana katika kufikisha taarifa kwa jamii ndiyo maana tunawashirikisha ili kupaza sauti zetu pale ambapo sisi tunahitaji zifike. Mradi wetu umefanya vitu vingi kwa ajili ya mradi huo wa elimu jumuishi," alisema

Pia alisema hivi sasa kuna Shule ya Msingi Bahi Sokoni mkoani hapa na Shule ya Msingi Nkuhungu Dodoma Jiji ambazo ni miongoni mwa shule za mfano katika utekelezaji wa mradi huo wa elimu jumuishi.

Mfumo wa Elimu Jumuishi unajumuisha wanafunzi wenye ulemavu wa aina mbalimbali kusoma na wanafunzi wa kawaida ili kuimarisha umoja na usawa katika mfumo huo.

Naye Mwanasheria wa Kujitegemea, Fredrick Mkatambo, alisema ziko changamoto zinazowakabili watoto wenye ulemavu ikiwamo kunyimwa haki za msingi kutokana na baadhi ya wazazi na walezi kuwa na dhana ya kwamba anapozaa mtoto mwenye ulemavu, ni mkosi au laana.

"Mambo haya nimeyashuhudia sio kwa nadharia tu lakini tumeyashuhudia, kwa mfano kuna mtoto mlemavu wazazi wake walitaka kumtupa kwenye mto ili achukuliwe na maji afe lakini babu yake na yule mtoto alisimama kidete kupinga hali ile. Aliamua kumchukua mjukuu wake na kumlea, leo hii mtoto yule ni mwandishi wa habari," alisema.

# BAKWATA yapiga 'stop; ndoa holela

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

BARAZA Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Wilaya ya Dodoma, limepiga marufuku walimu wasio waaminifu kuozesha ndoa za Kiislamu bila kufuata utaratibu unaotambuliwa.

BAKWATA pia imeagiza wale wote wanaofungisha ndoa za Kiislamu wahakikishe wanakuwa na vyeti halisi na leseni maalumu inayotambuliwa na baraza hilo.

Angalizo hilo lilitolewa jana na Katibu wa BAKWATA Wilaya ya Dodoma, Ahmed Msuri, alipokuwa akizungumza na mashekhe, maimamu na walimu kutoka kata mbalimbali kwenye kikao cha utendaji kilichofanyika kwa ajili ya uchangiaji wa mfuko maalumu wa Shekhe Mkuu wa Tanzania.

Katibu huyo alisema hivi sasa kumekuwapo na ufungishaji wa ndoa za Kiislamu holela zisizo halali ambazo hufungwa mitaani huku wakitumia vyeti bandia ambavyo havitambuliwi na BAKWATA.

Alisema hali hiyo imechangia kwa kiasi kikubwa kuwapo kwa migogoro mingi kwenye ndoa isiyo na tija, ambayo imekuwa ikishindikana kutatuliwa kutokana na wengi wao kubainika kuwa na vyeti feki.

Kutokana na hali hiyo, aliema BAKWATA Wilaya ya Dodoma kuanzia sasa inapiga marufuku walimu wasio waaminifu kufungisha ndoa hizo badala yake kwa zile zitakazojitokeza zitafungishwa na mashekhe na maimamu wa kata ambao wanatambuliwa kisheria na wana vibali.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya BAKWATA Wilaya ya Dodoma, Bashiru Hussein, aliwataka mashekhe na maimamu kujenga ofisi zao kwenye kata ili kutatua kasoro zinazojitokeza walimu wanapofungisha ndoa kwa kutumia vyeti feki.

Alisema ofisi hizo zikiwapo, wale wote watakaohitaji kufunga ndoa zao watakuwa wakiwafuata ili wapatiwe huduma hiyo.

Pia aliwataka mashekhe, maimamu wa misikiti na walimu wa madrasa kuhakikisha wanatoa elimu dhidi ya ugonjwa wa corona katika kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya na viongozi wa serikali za dini.



# Kasi maji yawakimbiza wawekezaji, wananchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BAADHI ya wawekezaji na wananchi wameyakimbia maeneo katika kijiji cha Jambiani, mkoa wa Kusini Unguja kutokana na maji kuvamia na kuharibu maeneo ya fukwe.

Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi Zanzibar, Riziki Pembe Juma, aliyasema hayo jana alipotembelea maeneo hayo na kuzungumza na baadhi ya wawekezaji na wananchi kuhusu tishio la maji ya bahari kuvamia maeneo ya makazi yao. Pembe alisema kasi ya maji ya bahari kuvamia maeneo ya fukwe ni sehemu ya athari za mabadiliko ya tabia ya nchi ambayo yameikumba dunia kwa ujumla wake.

Alisema utafiti uliofanywa na Mamlaka ya Mazingira Zanzibar umegundua kuwa yako maeneo 120 ambayo yameathirika na mabadiliko ya tabia ya nchi huku maji ya bahari yakitishia maisha ya wananchi wanaoishi pembezoni mwa bahari.

"Zanzibar ni kisiwa ambacho kinatajwa kukabiliwa na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi ambapo kasi ya maji ya bahari kuvamia maeneo ya makaazi ya wananchi wanaoishi pembezoni mwa bahari," alisema.

Haji Iddi, mwekezaji wa hoteli ya Jambiani Visitors Inn, alisema kasi ya maji ya bahari inatishia uhai wa maendeleo ya sekta ya utalii katika ukanda huo.

"Uhai wa hoteli za kitalii zilizoko pembezoni mwa fukwe za bahari eneo la Jambiani upo hatarini kutokana na kasi ya maji ya bahari kuvamia maeneo hayo," alisema.

Annaster Poter, raia kutoka Norway anayemiliki nyumba ya kulala wageni kijijini hapo, alisema miongoni mwa njia za kukabiliana na kasi ya maji ya bahari katika kijiji hicho ni kujengwa kwa ukuta utakaozuia kasi ya maji kuvamia maeneo ya makazi ya wananchi.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Mazingira Zanzibar, Sheha Mjaja, alikiri kuwapo kwa athari za tishio la maji ya bahari kuvamia maeneo ya makaazi ya wananchi wa kijiji cha Jambiani pamoja na hoteli zinazomilikiwa na wawekezaji.

"Mamlaka ya mazingira tunaendelea kufanya tathmini zaidi kuhusu njia ya kukabiliana na athari hizo ambapo katika hatua ya awali tunajuwa kwamba matatizo hayo yanatokana na mabadiliko ya tabia ya nchi," alisema.



Daktari wa Afya ya Mama na Mtoto, Ummkulthum Omar Hamad, akitoa mada ya afya ya uzazi kwa wanachama cha Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) Zanzibar, katika mkutano mkuu wa chama hicho, huko Tunguu Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mwinyi asisitiza ushirikiano, uzoefu TEHAMA

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameitaka Wizara ya Mawasiliano ya Teknolojia ya Habari ya serikali ya Muungano, kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ya Zanzibar ili kupeana uzoefu.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu jijini Zanzibar alipokutana na Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile na ujumbe wake waliofika kwa ajili ya kuitambulisha wizara hiyo mpya.

Alisema ushirikiano kwa wizara hizo mbili unahitajika hasa ikizingatiwa kwamba Zanzibar nayo ingependa kwenda kwa kasi katika sekta hiyo hivi sasa.

Rais alisema juhudi za makusudi zitaendelea kuchukuliwa na Zanzibar katika kuhakikisha malengo yaliyowekwa katika kuimarisha teknolojia ya habari yanafikiwa kwa ushirikiano wa pamoja kati ya wizara hizo mbili.

Naye Waziri Ndugulile alisema wizara hiyo imeanzishwa Desemba, mwaka jana katika maandalizi ya kuiandaa nchi kwenda katika uchumi wa kidijitali na mapinduzi ya viwanda sambamba na kutengeneza serikali ya kimtandao na biashara mtandao pamoja na sekta hiyo kuwa na mchango katika pato la taifa.

Kwa msingi huo, alisema Rais John Magufuli aliona ni muhimu kuwa na wizara ambayo itakuwa inashughulikia mawasiliano na teknolojia ya habari.

Alisema kwa vile baadhi ya majukumu ya wizara hiyo ni ya muungano, hivyo amekuja Zanzibar na ujumbe wake na kufanya mikutano ya ushirikiano na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ya Zanzibar na alifanya ziara kisiwani Pemba kwa ajili ya kuvitembelea vituo vya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA). Ndugulile alisema kikao chao na Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi wa Zanzibar kimekwenda vizuri na ana matumaini makubwa kwamba mafanikio makubwa zaidi yatafikiwa huku akieleza azma ya ziara yake aliyoifanya kwa upande wa Unguja na Pemba.

Kuhusu mradi wa anwani za makazi ambao unatekelezwa hapa Zanzibar, alisema wameamua kuuongezea kasi na kwamba umeanza kwa ngazi za majaribio hasa kwa Zanzibar kutokana na kuimarika sekta ya utalii.

# SMZ kuanzisha mfuko wa Mji Mkongwe

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imesema iko katika mchakato wa kuanzishwa kwa mfuko wa Mji Mkongwe ambao utawawezesha wananchi mbalimbali na wafadhili kuchangia maendeleo ya kuendeleza mji huo ambao uko katika orodha ya urithi wa dunia.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Lela Mohamed Mussa, alipohojiwa na Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) kuhusu maendeleo ya jengo la Beitl-al-jaib.

Alisema Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ambayo hujishughulisha na maendeleo ya utalii, imeanza mchakato wa kuweka utaratibu bora ambao utatumika katika kuundwa kwa mfuko utakaosimamia maendeleo ya Mji Mkongwe na uhifadhi wake.

Lela alisema uamuzi wa kuanzishwa kwa mfuko huo, umekuja ikiwa ni hoja iliyoibuliwa na wadau mbalimbali wakiwamo wa utalii waliohudhuria mkutano uloitishwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, baada ya kuporomoka kwa jengo la Beit-al-Jaib mwishoni mwa mwaka jana.

"Wizara imelipokea ombi la wadau wa sekta ya utalii kuhusu kuwapo kwa mfuko ambao wananchi watachangia kwa ajili ya kuendesha Mji Mkongwe. Ombi hilo tumelipokea ni zuri na tunalifanyia kazi," alisema.

Alisema mfuko huo utakuwa wazi ikiwamo matumizi ya fedha na njia za kuchangia. Alisema kazi kubwa inayokusudiwa kufanywa na wizara ni kuishajihisha jamii kuchangia kwa hiari kwa maendeleo ya Mji Mkongwe.

"Mfuko wa Mji Mkongwe utakaoanzishwa utakuwa wazi na huru kwa kila mwananchi au watu wenye uwezo kuchangia kwa ajili ya maendeleo ya ukuaji wa mji ambapo katika kipindi hichi tunataka kuhamasisha wananchi kuchangia kwa hiari," alisisitiza.

Pia alisema kwa sasa kazi za kuliweka jengo la Mji Mkongwe katika hatua za awali ikiwamo usafishaji wa eneo hilo, zinaendelea kwa ajili ya kuchukua tahadhari katika kipindi hiki cha mvua ili kuepuka athari zaidi za kuporomoka

Alisema mafundi wazalendo wanaendelea na kazi za ukarabati wa jengo hilo hadi kusubiri taarifa rasmi kutoka Oman kuhusu maendeleo ya jengo hilo pamoja na ukarabati wake.

"Tuliwauliza mafundi wetu kama jengo lile wanaweza kuliweka katika hali nzuri ili kusubiri tathmini zaidi na kuepuka athari za kuporomoka zaidi katika kipindi cha mvua kinachotarajiwa kuanza hivi karibuni na wao walitujibu wanaweza," alisema.

Jengo la Mji Mkongwe wa Zanzibar Beit-al-Jaib lilijengwa mwaka 1883 na utawala wa Sultani wa Oman, Barghashi, na sasa limetimiza takriban miaka 134 .

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI MACHI 13, 2021



**MAYD AJERUHIWA NA MOTO**
Ukurasa.14



## CHOZI LA AUNT EZEKIEL

# Wengi washangaa, wajiuliza kulikoni?

MWIGIZAJI mkongwe, Aunt Ezekiel, ameibua utata mwingine kufuatia kitendo chake cha kububujikwa na machozi mahakamani wakati watuhumiwa wa dawa za kulevya walipopandishwa kizimbani.

Watuhumiwa watatu wakiongozwa na Said Mbasha, walifikishwa katika Mahakama ya Kisutu, kujibu mashtaka ya kukutwa na kilo 30.6 za dawa ya kulevya aina ya Heroin.

Hata hivyo, wakati kesi hiyo ikiendelea msanii Aunt Ezekiel, alionekana akilia kwa kububujikwa na machozi muda wote huku watu waliokuwa karibu wakijaribu kumtuliza.

Baada ya video hiyo kusambaa kwa kasi katika mitandao ya kijamii, baadhi ya mashabiki wake walihoji kwa nini msanii huyo anaangua kilio na kama mmoja wa washtakiwa hao ni ndugu yake.

Aunt Ezekiel, mwenyewe hakutaka kutoa ufafanuzi kutokana na tukio hilo, badala yake wakati akitoka chumba cha mahakama alipanda gari na kuondoka bila kusema chochote.

"Yawezekana mmoja wa washtakiwa ni ndugu yake, lakini hakutaka kuweka wazi na jambo hili linatupa wasiwasi mashabiki wake," amesema Amina Juma wakati akichangia mjadala huo.

Said Mbasha (24), mkazi wa Mbezi Tangibovu, na wenzake watatu , walifikishwa mahakamani hapo wakikabiliwa na mashtaka ya kusafirisha dawa za kulevya aina ya Heroin kilo 30.

Wengine ni Joseph Dalidali (27), Allu Murugwa( 24) mkazi wa Kijitonyama na Fatima Shomari(24).

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon , akiwasomea mashtaka mbele ya Hakim Mkazi Mfawidhi, Godfrey Isaya, alidai washtakiwa wanadaiwa kutenda makosa yao, Machi 3, 2021 katika eneo la Kijitonyama Wilayani Kinondoni.


BASI SAWA

## Malaika kumbe ulikuwa mkaidi

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Malaika, amesema changamoto za kifamilia zinasababisha wasanii wa kike kuwa wachache katika muziki.

Malaika ameeleza kwa upande wake alijikuta anashindwa kuzungumza na baba yake kwa kipindi cha mwaka mzima baada ya kuamua kuingia katika fani hiyo.

"Mimi wakati naanza muziki nilimaliza mwaka mzima bila mazungumzo na baba yangu kisa alikuwa anaona kama uhuni, pili kumsimamia msanii wa kike ni kazi kuliko mwanamume kwa sababu tunagharama nyingi ndio maana watoto wa kike wanakuwa wachache kwenye muziki" ameeleza



## Stamina ampa tano mama Lionel

RAPA anayetamba kwa sasa, Stamina, amemtaja mama wa mtoto wake kuwa mpambanaji na wakati fulani alimsaidia kukusanya pesa katika shoo zake.

Akizungumzia hilo kwenye kipindi cha PlanetBongo ya East Africa Radio, Stamina amesema alishangazwa na kitendo hicho kwani hakutegemea kama mpenzi wake huyo atafanya jambo hilo kwa zaidi ya mikoa 15.

" Mama Lionel, kipindi nakutana naye sikutegemea kama ni mpambanaji, alinishangaza kwani nilikuwa na ziara zangu za chaka kwa chaka za mikoani akasema twende wote, yeye alikuwa anakaa getini kuchukua pesa wakati nafanya shoo kwenye jukwaa na alikuwa anawakazia " ameeleza Stamina.





# Tunda yani hata wababe walikushindwa!

MPAMBAJi wa video za muziki, Tunda, amemsifia mpenzi wake Whozu kuwa shabaki kutokana na kufanikiwa kuwa naye kimapenzi kwa miaka miwili, kitu ambacho wengine walishindwa.

Tunda ametoa sifa hizo wakati anasheherekea siku ya kumbukumbu ya kuzaliwa kwake, kupitia ukurasa wake wa Snapchat na Instagram amesema wanaume matajiri na wababe hawakumuweza.

"Miaka mitatu ya kukujua sijawahi kujutia, kukuchoka wala kutamani kuwa mbali na wewe, hongera kwa hilo mchaga sio jambo rahisi, walishindwa watu wababe hadi matajiri, Happy Birthday handsome boy wangu" ameongeza.

# Masikini wa macho; Kisebusebu na kiroho papo

**Na Adam Fungamwango**

KWENYE maisha ya kawaida, mtu anaweza kuona kama hakitaki kitu fulani, lakini akitokea mtu mwingine akisema anakihitaji, basi utaona yule alionekana hakitaki anabadili mawazo.

Hapa kwenye maisha ya ndoa, kuna wanaume au wake ambao wanawanyanyasa wenzao na kuonekana kama vile wanajipendekeza sana kwao, lakini inapotokea anasikia kuna mtu pembeni anamnyemelea, anageuka mbogo.

Hii ndiyo iliyosababisha waswahili kuwa na msemo wa 'kisebusebu na kiroho papo.'

Leo tunaiangalia filamu moja kabambe iitwayo 'Masikini wa Macho.' Ni filamu yenye mafunzo kwa jamii ambapo pia kama utaiangalia utafurahi, kuhuzunika na hata kulia.

Inamhusu jamaa mmoja aitwaye Denis ambaye ana mke wake wa ndoa. Anaitwa Rose. Baada ya kuoana miaka michache ikapita bila dalili zozote za kupata mimba, achilia mbali kupata mtoto.

Hili lilimfanya Denis ajione mnyonge. Akaanza kumnyanyasa mkewe. Ikafikia wakati akawa anamtukana na mwisho wake akamtimua nyumbani kwake.

Japo baada ya siku kadhaa mke alirejea na kuomba sana warudiane, lakini Denis alikataa katakata. Rose alisalimu amri akarudi kwao. Na huko wazazi wake walikuwa wamefariki, badala yake wanaishi dada na kaka yake tu.

Baada ya muda akampata kijana mmoja ambaye ni mlemavu wa macho. Hakujali hilo. Alichojali ni upendo wa dhati.

Kijana akamsimulia maswahibu yaliyomkuta nyuma kuwa alikuwa na wazazi wake, lakini walifariki akiwa mdogo, akalelewa na kaka yake.

Alipokuwa huko, mke wa kaka yake akamlazimisha afanye naye mapenzi. Alipokataa ndipo alipotengeneza uongo kuwa alitaka kumbaka.

Kama kusikia hivyo akamtimua mdogo wake nyumbani licha ya ulemavu alionao.

Habari hiyo ilizidi kumfanya Rose amuonee huruma kijana huyo mtanashati.


Mapenzi yao yalinoga, kiasi cha kuwashangaza wengi na kuwa kivutio pia. Kijana huyo aliitwa Lameck.

Habari ikamfikia Denis. Na kuna siku akawafuma laivu kabisa.

Akili ikamkaa sasa Denis na kumwomba mkewe warudiane. Mke alikataa katakata. Akamwambia sababu ambazo zilimfanya amtimue bado zipo. Denis akaunda kikundi cha maharamia kwa ajili ya kumteka Lameck na Rose pia.

Walitekwa, lakini walipelekwa sehemu tofauti. Rose nyumbani kwa Denis, Lameck porini, ikiwa ni pamoja na mateso makali.

Kutokana na hali yake ya upofu, mateso yanamshinda akafariki dunia.







# Rayvanny wewe 'Next Level'

OFISA Mtendaji wa lebo mpya ya muziki ya Next Level, Rayvanny, amesema kuanzisha kampuni yake si kwamba anataka kushindana, bali kuendeleza na kukuza vipaji vya wasanii.

Rayvanny amesema lengo ni kuona lebo zingine kama Konde Gang, Kings Music na WCB zinaendelea kusaidia vijana.

Hata hivyo, amesema hana nia ya kujitoa WCB bali anataka kupanua wigo na kuwafikia vijana wengi wenye vipaji.

# Kiambukuta mkongwe aliyeiacha Congo



**Na Adam Fungamwango**

MSHTUKO mkubwa uliwapata mashabiki wa muziki wa rhumba na dansi duniani, baada ya kupata taarifa za kifo cha mwanamuziki mkongwe nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Josky Kiambukuta.

Mkongwe huyo aliyefariki Jumapili ya Machi 7, mwaka huu, akiwa na miaka 72, ni mwimbaji kiongozi na mtunzi mahiri wa bendi ya TP OK Jazz iliyokuwa inaongozwa na Franco Lwambo Lwanzo Makiadi ambaye alifariki dunia mwaka 1989.

Taarifa zinasema kuwa Kiambukuta alifariki kwenye Hospitali Kuu jijini Kinshasa iitwayo, Ngaliema baada ya kuugua kwa muda mfupi kwa mujibu wa familia yake.

Mara ya mwisho alikuwa na kundi ya Bana OK, baada ya kifo cha Franco, lakini pia alikuwa akipiga muziki na wakongwe wenzake wakifanya ziara mbalimbali bara la Ulaya, Asia na Afrika.

Ni mwanamuziki aliyeanza kuvuma tangu miaka ya 1960, akiwa na kundi la Africa Fiasta Sukisa lililokuwa likiongozwa na Dk. Nico Kasanda wa Mikalayi. Alijiunga na TP OK Jazz mwishoni mwa miaka ya 1960 na kujizolea umaarufu mkubwa kutokana na sauti yake tamu, akitunga nyimbo mbalimbali na pia kuimba za wenzake.

Pamoja na kuwa na waimbaji wengi kwenye bendi hiyo, lakini anachukuliwa ni mmoja kati ya waimbaji viongozi na nembo ya bendi.

Ameimba na kutunga nyimbo nyingi sana, lakini leo tutaziangalia nyimbo tano maarufu kwa mashabiki wa muziki wa dansi ambazo ametunga na kuimba pia.

**Monzo-1974**

Ni moja kati ya nyimbo zilizompatia umaarufu na kumpa heshima kubwa kwenye bendi ya TP OK Jazz, chini ya Franco.

'Monzo', ulikuwa ni wimbo maarufu sana katikati ya miaka ya 1970, baada ya kuutunga na kuutoa mwaka 1974, ukipigwa kila kona, hata hapa nchini Tanzania.

Gitaa kali staili ya 'kente', ilichangia wimbo huo kupendwa sana na mashabiki.

**Fariya-1977**

Mwaka 1977, alikuja na kibao kimoja alichokiita 'Fariya' ambacho nacho kilizidi kumfanya kuwa mmoja wa wanamuziki tegemeo na wenye heshima kubwa kwenye bendi hiyo, licha ya kwamba kulikuwa na waimbaji wengi kwenye bendi hiyo.

**Missile-1983**

Jamaa alikuwa habahatishi. Mwaka 1983, aliibuka na kibao kingine kilichopendwa sana kilichokuwa na jina la 'Missile'.

Kilipigwa na staili ya taratibu, lakini kinachopendeza mno masikioni, pamoja na yenye mwenyewe kuimba kwa huzuni, akighani kwa hisia kali sana, huku gitaa likipigwa kwa kubembeleza.

**KSK-1984**

Mwaka mmoja baadaye alitunga wimbo mmoja ulitwao 'KSK' na kuzidi kujijengea heshima ya kuwa mwimbaji mwandamizi kwenye bendi hiyo.

**Chadra Dechade-1989**

Huu ndiyo mwaka ambao Franco alifariki. Na ndiyo mwaka ambao alitoa kibao maarufu sana kiitwacho 'Chandra Dechade.'

Hadi leo huwa kinapigwa kwenye bendi nyingi zinazopiga muziki wa laivu. Ni moja kati ya nyimbo zake ambazo zilinyanyasa sana mwanzoni mwa miaka ya 1990, hadi leo hii ukipigwa, watu wanaacha viti vyao. Madilu System pia ana kipande chake alichoimba kwenye wimbo huu.



# Maskini wamemponza Eric Omondi

OFISA Mkuu Mtendaji wa Bodi ya Ukaguzi Filamu nchini Kenya (KFCB), Dk. Ezekiel Mutua, amethibitisha kukamatwa kwa mchekeshaji maarufu nchini humo, Eric Omondi, baada ya kukiuka kanuni ya maadili ya bodi hiyo.

"Maofisa wa Ufuatiliaji wa Bodi ya Uainishaji wa Filamu Kenya wakishirikiana na Polisi kutoka Kurugenzi ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) wamemkamata Eric Omondi kwa kukiuka masharti ya Sheria ya Filamu na Maonyesho ya Sura, Sura 222 ya Sheria za Kenya kwa kutengeneza na kusambaza filamu ambayo haijaidhinishwa," amesema Mtendaji huyo.

Filamu ambayo mchekeshaji huyo amekiuka kuitoa ni "Wife Materia." inayojumuisha wahusika kutoka Kenya na Tanzania wanaoonekana wakipigana hadharani na kulazimu Polisi kuingilia kati.



## Car B apata 'dhahabu' wimbo wake

MSANII wa Marekani, Cardi B amevunja rekodi kwa kuwa rapa wa kwanza mwanamke kuchukua tuzo ya dhahabu baada ya wimbo wake kuuzwa nakala nyingi.

Singo yake ya 'Bodak Yellow' imefanikiwa kuuzwa nakala milioni 10 kupitia viwango vya RIAA na kumfanya kufikia hadhi hiyo.

Kulingana ukurasa wa twitter, Chama cha Rekodi ya Marekani ( (RIAA) kimempongeza mwanamuziki huyo kuwa mwanamke wa kwanza kupata tuzo hiyo kupitia wimbo wake uliorekodiwa na AtlanticRecords.

## Khloe abadili sura yake?

MWANAMITINDO Khloe Kardashian, ameibua mjadala mkali baada sura yake kuonekana tofauti na ilivyokuwa nyuma.

Khloe aliweka video yake mpya katika mitandao ya kijamii na kuzusha gumzo baada ya baadhi ya wafuasi wake kuhoji utofauti huo na kumuuliza kama alifanya upasuaji wa kubadilisha mwonekano.

Mashabiki hao walikwenda mbali kwa kusema mshiriki huyo wa kipindi cha maisha katika televisheni anautumia utajiri wake vibaya kwa kujibadilisha mwonekano kama wanavyofanya mastaa wengi wa Marekani.







## MayD ajeruhiwa na moto

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Akinmayokun Awodumila, maarufu kama MayD, amelazwa hospitali baada ya kujeruhiwa na moto.

Nyota huyo kupitia ukurasa wake wa Instagram, aliweka picha zilizomwonyesha amelazwa hospitali kutokana na majeraha ya ajali ya moto nyumbani kwake.

"Wapendwa tafadhali niombeeni nimepata ajali ya moto nyumbani kwangu, nimepata majeraha ya kuungua," ameandika MayD.

## Ka3na hana ushamba kivile

MSHIRIKI wa shindano la Big Brother Naija, Ka3na Jones, ametolea ufafanuzi nyumba yake mpya, akieleza ameinunua kabla ya kushiriki shindano hilo.

Kauli hiyo ameitoa baada ya mshiriki mwenzake, Nengi, kuiposti nyumba hiyo na kuandika kuwa makazi mapya ya Ka3na yaliyopo jijini Lagos.


"2021 nilifanya vizuri, hii inatokana na kufanya kazi ngumu na hatimaye kuongeza orodha ya mali zangu, namshukuru Mungu kwani nilinunua kabla sijaingia ndani ya nyumba," amesema Ka3na



MAKALA

# PERSEVERANCE ROVERS
# Chombo kinachofichua mengi sayari ya Mars

**Mwandishi Wetu**




Chombo cha Perseverance Rovers kikiendelea kufanya uchunguzi katika sayari ya Mars

CHOMBO kilichopewa jina la Perseverance Rover, kinaendelea kuichunguza sayari ya Mars, kwa kuleta picha mpya zinazoonyesha mazingira halisi ya sayari hiyo nyekundu.

Katika kipindi cha wiki tatu tangu kitue salama katika sayari hiyo, chombo hicho kimetuma picha kadhaa ambazo wanasayansi wanazitumia katika kuchunguza ziwa kubwa lililopo katika bonde linalofahamika Jezero.

Katika hali ya kushangaza, hivi karibuni Perseverance Rover, kupitia kifaa chake kinachoitwa SuperCam, imetuma sauti ya miamba inayosuguana kwa mara ya kwanza.

Chombo hiki chenye mwangaza mkubwa kinaweza kutambua miamba iliyopo mbali na kuifanyia uchunguzi.

Mbinu hiyo ilitumiwa na chombo cha awali cha Nasa kinachoitwa, Curiosity, lakini haikutoa matokeo ya kufurahisha.

Hata hivyo, Perseverance kimeimarishwa zaidi kiuwezo, ikiwa ni pamoja na kuwekewa kinasa sauti ambacho kinawezesha kusikiliza sauti za mashine yake na jinsi inavyofanya kazi.

Hili halikufanyika kwa misingi ya kupata picha bora tu za sayari ya Mars, wala kwa lengo pia la kujinadi, bali kutoa taarifa za ziada ambazo ni muhimu kwa wanasayansi.

Sauti za mashine hiyo ikigonga mwamba inafichua ujuzi kama vile ugumu wa maeneo yanayolengwa wakati inachunguza sayari hiyo ya Mars.

"Kama tukigusa sakafu ambayo ni ngumu, hatutasikia sauti sawa na itakapoguswa eneo ambalo ni laini ," anafafanua Naomi Murdoch, kutoka katika Taasisi ya wataalamu wa anga za mbali ya Ufaransa , iliyopo mjini Toulouse.

"Chukua kwa mfano chaki au mwamba.Vitu hivi vinamchanganyiko wa kemikali unaofanana, lakini vina mchanganyiko tofauti kabisa wa kifizikia ."

Katika mkutano na waandishi wa habari siku ya Jumatano, Dk. Murdoch alicheza sauti tatu tofauti zilizorekodiwa na kinasa sauti cha SuperCam zilizochukuliwa kutoka sayari ya Mars.

Sauti moja ilikuwa ni sauti ya jumla ya kawaida ya Mars, ya pili ilikuwa ya upepo, na ya tatu ilikuwa ni ya mapigo yaliyosikika wakati wa upasuaji wa mwamba.

Chombo hicho-Perseverance kilitua kwenye shimo la maji lililopo Mars Februari 18, mwaka huu kwa ajili ya kutafuta ushahidi wa uwepo wa maisha ya nyakati zilizopita.

Shimo hilo lenye kina kirefu linachukuliwa kama mahali pazuri zaidi kwa ajili ya utafiti huo, kwasababu limekuwa na ziwa kwa miaka mabilioni iliyopita.

Inaaminika mahali palipo na maji huenda kutakuwa na uhai.

Kifaa cha SuperCam kilitengenezwa kwa ushirikiano wa timu ya watafiti wa Ufaransa na Wamarekani.Kifaa cha kwanza kilicholenga utafiti wa miamba kilipewa jina "Máaz", ikimaanisha Mars kwa lugha ya Navajo inayozungumzwa na Wamarekani wazawa wanaoishi maeneo ya kusini magharibi mwa nchi hiyo.

Haikumshangaza kwamba Mars ilikuwa na asili ya miamba, kwani hali hiyo ni kitu cha kawaida katika sayari hiyo.

Sauti hiyo ilitokana na mwamba ambao una kiwango kikubwa cha madini ya magnesium na chuma, madini haya hutokana na mlipuko wa lava iliyopoa kwa haraka.

"Hatujafahamu bado kama miamba hii yenyewe iko hai, mfano volcano, au labda ni miamba iliyoundwa na mimea iliyosombwa na mito hadi kwenye maji ya ziwa Jezero na kujikusanya pamoja ," anaeleza Mkuu wa Uchunguzi wa SuperCam, Roger Wiens, kutoka maabara ya kitaifa ya Los Alamos iliyopo New Mexico.

"Tutahitajika kutumia mbinu zetu zaidi na kujifunza kuhusu maeneo yanayozingira eneo hilo ili kuelewa mambo zaidi,"anaongeza kusema.

Perseverance kimeanza kujiendesha chenyewe kuelekea maeneo ya kaskazini mashariki katika sayari hiyo.

Hata hivyo, lengo ambalo bado halijatimia ni kurusha helikopta ndogo kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Chombo hicho kiliwekewa helikota ndogo kutoka duniani kwa ajili ya kusaidia kazi hiyo, kutokana na gari hilo linaweza kuangalia eneo tambarale linalofaa ambako helikopta hiyo yenye uzito wa kilo mbili, inayoitwa Ingenuity, inaweza kuwekwa kwa usalama ardhini. Kwa sasa helikota hiyo ndogo imeshikizwa kwenye sehemu ya chini ya Perseverance.



Sehemu ya miamba inayopatikana sayari ya Mars

# TASAF YAMNUSURU MAMA ALIYETELEKEZWA

**Na Lilian Lugakingira,** Mwanza

## •Kutoka upondaji kokoto hadi kumiliki kiwanja
## •Nyamagana yawa mfano kuinua kaya maskini



Euzebia Majia akiwa katika shughuli zake za kuhudumia mifugo

NILIBATIZWA jina na kuitwa mwenye shida, kutokana na kazi nilizozifanya za kuponda kokoto na kubeba zege, ambazo wengine waliona ni udhalilishaji" anasema Euzebia Majia mkazi wa Mtaa wa Iseni, Kata Butimba, Wilaya ya Nyamagana mkoani Mwanza.

Mama huyo mwenye umri wa miaka 48, ana watoto sita ambao wako katika hatua mbalimbali kimasomo. Anasema alitelekezwa na mume wake na sasa anaishi katika chumba kimoja kidogo akiwa na watoto wake.

Anasema, kutokana na maisha ya shida aliyoishi mtaani, ulipofika mpango wa kunusuru kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) awamu ya kwanza, jina lake lilipigiwa kura na idadi kubwa ya wananchi wa mtaa mzima.

"Wakati wahusika wa TASAF wamefika mtaani sikuwepo nyumbani, niliendа kuhangaika kutafuta riziki ya watoto wangu, lakini kwa kuwa nilifahamika ninavyoishi maisha ya shida na wanangu, kila mtu alinipigia kura niingizwe kwenye mpango" anasema.

Anaeleza sasa ana miaka mitano tangu aingizwe katika mpago huo wa kunusuru kaya maskini.

"Kabla nilikuwa na maisha magumu sana lakini sikukata tamaa, nilipambana kufanya kazi yoyote ile ilimradi nipate kipato kwa ajili ya kuwapatia watoto wangu mahitaji" anaendelea kusema.

Euzebia anasema ruzuku ya kwanza alipewa Sh. 64,000 na kuwa alitumia fedha hizo kununua mawe kwa ajili ya kuponda kokoto na kununua mchele kwa ajili ya kupika vitumbua vya kuuza.

"Kabla sijaanza kupata hiyo ruzuku nilikuwa nampondea mtu kokoto na kupata ujira kidogo, lakini baada ya kuanza kupata ruzuku nilinunua mawe yangu ambayo niliponda kokoto mwenyewe na kuuza, kwa hali hii kipato kiliongezeka kidogo" anaongeza.

Baada ya miaka mitatu alinunua kuku na bata na kuanza kufuga, na kwamba ameendelea na ufugaji huo wa kibiashara hadi sasa.

"Pamoja na kuanza kufuga kuku na bata, sikuacha kazi yangu ya kuponda kokoto bali niliachana na ubebaji wa zege, lakini pia niliendelea kutengeneza vitumbua na kuuza hadi nikawa maarufu mtaani kama vitumbua" anasema.

"Baadae nilipata pesa nikanunua kiwanja ambacho gharama yake ni Sh. milioni 1.3 kwa kulipa kwa awamu, mwenye kiwanja alinisaidia sana hata nilipopata Sh. 20,000 nilimpa kupunguza deni na aliipokea na kuandika kwenye daftari" anasema.

Anasema kwa sasa ruzuku anayopokea imepunguzwa kutoka Sh. 64,000 hadi Sh. 48,000 kiasi ambacho bado anaona ni msaada mkubwa kwake.

Anasema mfuko huo pia umemuwezesha kusomesha mtoto wake wa kwanza anayesoma chuo cha kati kwa miaka mitatu na sasa yuko mwaka wa kwanza, huku wa mwisho akisoma darasa la tano.

Anatumia fursa hiyo kuwaasa wanufaika wengine wa TASAF kuwekeza kidogo fedha wanazozipata kwa kufanya ufugaji na miradi mingine midogo, badala ya kuzitumia zikaisha na kukaa kusubiria ruzuku inayofuata.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Iseni, Slyvester Makunami, anasema wanufaika katika mtaa wake walipatikana kwa kuitisha mkutano na kuwaorodhesha wahitaji kutoka katika kaya maskini na baada ya hapo orodha iliyopatikana ilikabidhiwa kwa maofisa wa TASAF.

"Baadae tuliletewa orodha ya wanufaika ambao walipigwa picha na kuanza kunufaika, wapo fukara kabisa ambao tuliwaorodhesha awali lakini majina yao hayakurudi, hili limetuletea malalamiko kwamba viongozi tumeshiriki kuwaondoa" anasema.

Aidha mwenyekiti huyo analalamikia kiwango cha fedha wanachopewa wanufaika kimekuwa kikipunguzwa bila kupewa taarifa, na kuwa wao kama viongozi wakiulizwa hukosa majibu.

"Tunaomba yanapotokea mabadiliko kama haya viongozi tufahamishwe ili tukiulizwa tuwe na majibu" anasisitiza.

Utekelezwaji wa mpango huo katika mtaa wake ulianza mwaka 2015 wakiwa na walengwa 75, lakini walipunguzwa hadi kufikia 41 kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kifo, kuhama mtaa na wengine kuondolewa wakati wa uhakiki.

"Sh. milioni 55.5 zimekwishaletwa katika mtaa wetu kusaidia kupunguza hali ya umaskini, lakini pia zimesaidia kuongezeka kwa mahudhurio ya watoto shuleni na kliniki" anasema mwenyekiti huyo.

Hata hivyo, kiongozi huyo anaeleza awali wananchi wa mtaa huo walidharau kuhudhuria mikutano ilipoitishwa, lakini baada ya kuona kazi kubwa iliyofanywa na serikali kupitia TASAF maudhurio yanakuwa makubwa kwenye mikutano.

Amadeus Kamagenge, ambaye ni Mkurugenzi wa Programu za Jamii wa TASAF, anasema baada ya kukamilika kwa kipindi cha kwanza cha TASAF awamu ya tatu, hatua ya pili ilianza mwaka 2020 na itakamilika 2023.

Kamagenge anasema katika kipindi cha pili utaratibu wa utoaji wa ruzuku kwa kaya maskini utabadilika, mfano kwa kaya zenye watu wenye nguvu za kufanya kazi hawatapata ruzuku bali watapaswa kufanya ajira za muda na kupewa ujira.

"Sio kwamba katika kipindi cha kwanza cha TASAF awamu ya tatu hakukuwa na ajira za muda, zilikuwapo lakini katika baadhi ya wilaya na baadhi ya maeneo, kwa sasa zitashushwa kwa takribani vijiji vyote" Kamagenge anasema.

Anasema chini ya utaratibu huo mpya kila kijiji itabidi kutengeneza miradi ambayo itawezesha kupatikana kwa ajira za wananchi wenye nguvu kutoka katika kaya maskini.

"Hawa watu watakuwa wakilipwa wastani wa Sh. 30,000 kwa mwezi" anasema.

Kuanzia Januari zoezi litaanza na ifikapo Juni mwaka huu utambuzi wa walengwa utakamilika, baada ya hapo watu wanaokusudiwa watanufaika.

Aidha anasema pamoja na utaratibu huo mpya, asilimia 20 ya kaya zinazohudumiwa na TASAF zinatarajiwa kuwa na hali nzuri kiuchumi na zitaondolewa katika mpango huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Ladislaus Mwamanga , anasema wakati kipindi cha kwanza cha mpango huo awamu ya tatu kikikamilika, wanafunzi 1,648 ambao hawakuwa na uwezo wa kwenda shule wamefanikiwa kutimiza ndoto zao.Mwamanga anasema wanafunzi 480 walifaulu kwenda sekondari.

"Pia watoto 377 walifaulu kwenda vyuo vikuu na kupewa mikopo na bodi ya mikopo, bila huu mpango watoto hawa wa kaya maskini wasingefikia hatua hiyo ya elimu, na ndoto zao zingepotea.

HABARI KIMATAIFA

# Wanafunzi wa chuo watekwa Nigeria

**ABUJA,** NIGERIA

WATU wenye silaha Kaskazini Magharibi mwa Nigeria wamewateka nyara wanafunzi 30 jana usiku, katika Chuo cha Misitu kilichopo karibu na chuo cha jeshi.

Wanafunzi watatu walisema kuhusu tukio hilo ambalo ni la nne la wanafunzi kutekwa shuleni tangu Desemba, mwaka jana.

Chuo cha Shirikisho cha Mitambo ya Misitu kipo nje kidogo ya mji wa Kaduna katika mkoa uliozungukwa na magenge yenye silaha, ambayo mara nyingi hutumia usafiri kwa pikipiki.

Kamishna wa Usalama wa jimbo la Kaduna, Samuel Aruwan, alithibitisha shambulio hilo ingawa hakusema ni wanafunzi wangapi wamechukuliwa.

Sani Danjuma, mwanafunzi katika chuo hicho, alisema waliotekwa nyara wote walikuwa wanafunzi wa kike, licha ya mamlaka kutothibitisha hilo.

Wanafunzi wengine walisema baadhi ya wanawake walitoroka wakati wa shambulio hilo.

Mkazi wa eneo hilo, Haruna Salisu, akizungumza kwa njia ya simu, alisema alisikia milio ya risasi mara kwa mara saa 11:30 jioni.

"Hatukuwa na hofu, tukifikiri kwamba ilikuwa zoezi la kawaida la kijeshi lililokuwa likifanywa katika Chuo cha Ulinzi cha Nigeria," alisema.

"Tulitoka kwenda maombi ya alfajiri, saa 11:20 asubuhi, na tukawaona baadhi ya wanafunzi, walimu na wafanyakazi wa usalama kote kwenye eneo la shule.

Walituambia kwamba watu wenye silaha walivamia shule na kuwateka nyara baadhi ya wanafunzi."

Salisu alisema aliona wanajeshi wakiwapeleka wanafunzi waliosalia kwenye chuo hicho.

Ijumaa asubuhi, jamaa za wanafunzi walikusanyika kwenye maeneo ya chuo hicho, ambacho kilikuwa kimezungukwa na malori karibu 20 ya jeshi.

Ni wiki chache zilizopita, wasichana wa shule 279 waliachiliwa baada ya kutekwa nyara kutoka shule ya bweni huko Jangebe Kaskazini Magharibi mwa jimbo la Nigeria la Zamfara.

Pia wavulana 27 waliachiliwa baada ya kutekwa nyara kutoka shule yao katika jimbo la Kaskazini katikati mwa Niger, pamoja na wafanyakazi watatu na wanafamilia 12.

Mwanafunzi mmoja aliuawa kwa kupigwa risasi katika shambulio hilo.

Jaribio la jeshi na polisi kukabiliana na magenge halijafanikiwa, wakati watu wakiwa na wasiwasi kuwa mamlaka ya serikali inawaacha watekaji nyara bila kuwaadhibu, kuwalipa kama ilivyotokea Zamfara.

Mwishoni mwa mwezi Februari, Rais Muhammadu Buhari alizionya serikali za majimbo kupitia sera yao ya kuwazawadia majambazi pesa na magari, akionya kuwa sera hiyo inaweza kuibuka mbaya.

Machafuko hayo yanaleta shida ya kisiasa kwa Buhari, jenerali mstaafu na mtawala wa zamani wa jeshi ambaye anakosolewa juu ya kuongezeka kwa uhalifu wa vurugu.

**REUTERS**



Mfalme Goodwill Zwelithini (kulia) wa jamii ya Wazulu nchini Afrika Kusini, aliyefariki dunia jana katika Hospitali ya KwaZulu-Natal, akipatiwa tiba ya kisukari, alikuwa kiongozi wa kabila kubwa zaidi nchini humo na kiongozi mashuhuri wa kitamaduni tangu mwaka1968. **PICHA: BBC**

# Ulaya yasitisha AstraZeneca

**COPENHAGEN,** DENMARK

BAADHI ya mataifa kadhaa ya Ulaya yamesimamisha kutumia chanjo ya COVID-19 ya AstraZeneca, baada ya ripoti kuwa chanjo hiyo ilisababisha kuganda kwa damu.

Miongoni mwa nchi hizo ni Denmark, Iceland na Norway.

Hata hivyo, mataifa hayo yalijizuia kusema moja kwa moja kuwa chanjo hiyo ndio sababu ya tatizo hilo la kuganda kwa damu. Denmark ilisema itasitisha utoaji wa chanjo ya AstraZeneca kwa siku 14, na Waziri wa Afya, Magnus Heunicke, alisema kwa wakati huu hawawezi kusema kwa uhakika kuwa chanjo hiyo ina uhusiano na tatizo hilo la damu.

Mtaalamu wa tiba ya maradhi yanayosababishwa na virusi kutoka taasisi ya magonjwa ya kitropiki iliyoko mjini London, Polly Roy, aliiambia DW kuwa huenda tatizo hilo halina uhusiano na chanjo yenyewe, bali matatizo waliyokuwa nayo wagonjwa walioathirika.

**DW**

## UN yahofia njaa Afrika

**NEW YORK,** MAREKANI

MAMILIONI ya watu duniani, baadhi yao katika nchi za Afrika , wanakabiliwa na hatari ya kufariki kutokana njaa inayosababishwa na mizozo, janga la corona na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres alionya.

Zaidi ya watu milioni 30 katika maeneo kama vile ya Sahel, pembe ya Afrika, Sudan Kusini, Yemen na Afghanistan yanakaribia kutangaza janga la njaa.

"Bila ya hatua ya haraka kuchukuliwa, mamilioni ya watu wataangamia kutokana na njaa," Guterres aliliambia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa wakati wa mkutano wa kujadili masuala ya chakula na usalama. Nchini Sudan Kusini, Guterres alisema asilimia 60 ya watu wanaendelea 'kukabiliwa na njaa.

Alisema Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ilikabiliwa na uhaba mkubwa wa chakula mwaka jana, huku karibu watu milioni 21.8 wakikumbwa na baa kubwa la njaa kati ya mwezi Julai na Desemba.

Mkuu wa UN pia alielezea wasiwasi wake kuhusu hali katika Jimbo la Tigray, Ethiopia, ambako msimu wa mavuno ulikatizwa na ukosefu wa usalama na ghasia, maelfu ya watu huenda wanakabiliwa na njaa.

**BBC**

## Algeria yaitisha uchaguzi

**ALGIERS,** ALGERIA

RAIS wa Algeria, Abdelmadjid Tebboune amesaini sheria inayoitisha uchaguzi wa awali wa bunge June 12, mwaka huu baada ya kulivunja bunge mwezi uliopita.

Uchaguzi wa bunge ulikuwa umepangwa kufanyika mwaka 2022, lakini mwezi Februari, Rais Tebboune alilivunja bunge na kuomba uchaguzi mwingine ufanyike kabla ya mwaka huu kama sehemu ya mageuzi.

Tebboune aliachia huru dazeni ya wanaharakati wanaotetea demokrasia wa vuguvugu la Hirak lililoandaa maandamano ya mabadiliko, ambalo lilimlazimisha mtangulizi wake Abdelaziz Boutlefika kujiuzulu mwaka wa 2019.

Uchaguzi unaokuja wa bunge utafanyika chini ya sheria mpya ya uchaguzi, ambayo iliidhinishwa na Rais Tebboune, taarifa kutoka ofisi yake ilisema.

Mwezi uliopita, Tebboune aliahidi kuwa uchaguzi hautakuwa na ufisadi, na utafungua milango ya bunge kwa vijana, akiongeza kuwa lazima vijana wawe na uzito wa kisiasa.

Maandamano yalionekana kama mwamko, kukiwa na maandamano mengine kote nchini, baada ya kusitishwa mwaka jana kufuatia masharti ya kupambana na janga la corona.

Waandamanaji wanaomba mabadiliko kamili ya mfumo wa uongozi uliopo tangu Algeria ijitapitie uhuru kutoka kwa Ufaransa mwaka wa 1962, na kumalizika kwa ushawishi wa jeshi katika taifa hilo la Kaskazini mwa Afrika.

**VOA**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Uza,
Chenye Thamani Kubwa
Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MWANAMISI AZIZI MOHAMEDI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.2297/0034** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **NDORWE SEKONDARI** mwaka **2013.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **WMB/RB/116/2020.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**Kinywele Magembe Ginassa** anatangaza kupoteza kadi yake ya pikipiki aina **SANLG** yenye namba za usajili T 607 BVS, Injini namba **LBRSPJB5XB9011911, chassis namba SLI57FMI 11937506.** Anaomba yoyote atakayekuwa ameiokota aiwasilishe katika kituo cha polisi Bariadi.
Taarifa imetolewa kituo cha polisi kwa namba **BRA/RB/1722/2012 ERV 46267748.**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
LAND DIVISION AT BUKOBA
LAND CASE APPEAL NO. 13 OF 2019**

**(From the decision of the District Land and Housing Tribunal of Bukoba District in Land Appeal No. ......... of ............ 200........... and Original Ward Tribunal of ..........Ward application No.....of 200......)**

**BRAISON DAMIAN ...........................APPELLANT**
**VERSUS**
**ANDASON DAMIAN.........................RESPONDENT**

**TO ANDASON DAMIAN
C/O WEO - BUGANGUZI WARD**

**NOTICE OF DATE OF HEARING**

TAKE NOTICE that the above case has been fixed for Hearing on the 20 day of April 2021 at 9:00 am before Hon. Dr. Ntemi Judge.
You are required to appear in this Court on the fixed date without fail.
Coppy of the petition of appeal of apper is attached here to and you may file your reply thereto into two days prior to the fixed date of hearing and serve a copy to the appellant.
Given under my Hand and the seal of the Court this 10 day of March 2021.

..................................................
**REGISTRAR**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
LAND DIVISION AT BUKOBA
LAND CASE APPEAL NO. 13 OF 2019**

**(From the decision of the District Land and Housing Tribunal of Bukoba District in Land Appeal No. ...............of................200..............and Original Ward Tribunal of ............Ward application No............of 200......)**

**BRAISON DAMIAN .............................APPELLANT**
**VERSUS**
**DAMIAN LAZARO............................RESPONDENT**

**TO DAMIAN LAZARO
C/O WEO - BUGANGUZI WARD**

**NOTICE OF DATE OF HEARING**

**TAKE NOTICE that the above case has been fixed for Hearing on the 20 day of April 2021 at 9:00 am before Hon. Dr. Ntemi Judge.
You are required to appear in this Court on the fixed date without fail.
Coppy of the petition of appeal of apper is attached here to and you may file your reply thereto into two days prior to the fixed date of hearing and serve a copy to the appellant.
Given under my Hand and the seal of the Court this 10 day of March 2021.**

..................................................
**REGISTRAR**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
LAND DIVISION AT BUKOBA
LAND CASE APPEAL NO. 13 OF 2019**

**(From the decision of the District Land and Housing Tribunal of Bukoba District in Land Appeal No. ...............of................200...............and Original Ward Tribunal of ............Ward application No............of 200......)**

**BRAISON DAMIAN .........................APPELLANT**
**VERSUS**
**JENIVA DAMIAN...............................RESPONDENT**

**TO JENIVA DAMIAN
C/O WEO - BUGANGUZI WARD**

**NOTICE OF DATE OF HEARING**

TAKE NOTICE that the above case has been fixed for Hearing on the 20 day of April 2021 at 9:00 am before Hon. Dr. Ntemi Judge.
You are required to appear in this Court on the fixed date without fail.
Coppy of the petition of appeal of apper is attached here to and you may file your reply thereto into two days prior to the fixed date of hearing and serve a copy to the appellant.
Given under my Hand and the seal of the Court this 10 day of March 2021.

..................................................
**REGISTRAR**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
LAND DIVISION AT BUKOBA
LAND CASE APPEAL NO. 13 OF 2019**

**(From the decision of the District Land and Housing Tribunal of Bukoba District in Land Appeal No. ...............of................200..............and Original Ward Tribunal of ............Ward application No............of 200......)**

**BRAISON DAMIAN ...........................APPELLANT**
**VERSUS**
**MWEBEMBEZI DAMIAN...................RESPONDENT**

**TO MWEBEMBEZI DAMIAN
C/O WEO - BUGANGUZI WARD BISHAKA**

**NOTICE OF DATE OF HEARING**

TAKE NOTICE that the above case has been fixed for Hearing on the 20 day of April 2021 at 9:00 am before Hon. Dr. Ntemi Judge.
You are required to appear in this Court on the fixed date without fail.
Coppy of the petition of appeal of apper is attached here to and you may file your reply thereto into two days prior to the fixed date of hearing and serve a copy to the appellant.
Given under my Hand and the seal of the Court this 10 day of March 2021.

..................................................
**REGISTRAR**

**NOTISI YA KUFUNGA KAMPUNI
ASEEL GROUP LIMITED
KAMPUNI NAMBA 73852
NOTISI YA MWEZI DESEMBA 2020**

MWENYEKITI ALIITISHA KIKAO KAMA ILIVYOSTAHILI NA WAHUSIKA WOTE WALIKUWEPO NA MKUTANO HUO ULIFANYIKA TAREHE 20 DESEMBA, MWAKA 2020, SAA 5:00 ASUBUHI NA MAKUBALIANO YAFUATAYO YALIFIKIWA:
WAHUSIKA WALIKUBALIANA KATIKA KIKAO HICHO KWA HIYARI YAO KUWA KAMPUNI HIYO IWE IMEFUNGWA TOKA TAREHE YA KIKAO 20/12/2020 NA HAKUTAKUWA NA BIASHARA YEYOTE AMBAZO ZITAKUWA ZINAENDESHWA KWA JINA AU KATIKA KAMPUNI.
KAMA MWANAHISA YEYOTE ATAKUWA NA LOLOTE JUU YA MAAMUZI HAYA ANATAKIWA AANDIKE BARUA YA KUPINGA MAAMUZI HAYA KWA MSAJILI WA MAKAMPUNI BRELA NDANI YA SIKU 21 KUTOKA TAREHE YA NOTISI HII.
HIVYO BASI MWENYEKITI ALITOA TAMKO KWAMBA HAKUTAKUWA NA BIASHARA YOYOTE ITAKAYOENDESHWA KATIKA KAMPUNI.

**MKUTANO ULIFUNGWA MNAMO SAA 8:30 MCHANA.
MAHALI: ARUSHA
Tarehe: 20/12/2020**

**ABDUL KARIM AHMAD DAKIK
Mwenyekiti wa Bodi**

**BERNAD BUBERWA BUHOMA
Sekretari wa Bodi**




**MUGABO AUCTION MART & COMPANY LIMITED**
P.O.Box 766 Musoma Tanzania.
Mobile: +255 755 555 295 | +255 673 672 848
Email: mugaboauction@gmail.com | Tell: 028 262 261

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MUSOMA MJINI
SHAURI LA TALAKA NA. 07/2019
RHOBI P. SAMWEL…………………………………………....MDAI
DHIDI YA
BONIPHACE M. MASERO………………………………...MDAIWA
KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA MWANZO MUSOMA MJINI TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA NYUMBA MALI YA WANANDOA KAMA IFUATAVYO:

| S/NO | MALI INAYOUZWA | MAHALI ILIPO | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | NYUMBA KWENYE KIWANJA NA.313 KITALU "V" MUTEX | MACHINJIONI, MUSOMA | SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA 19/03/2021 |

**MASHARTI YA MNADA:**

1. MTEJA ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO (25%) YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATALIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14), KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.
2. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

**MAWASILIANO
0755 555 295/0673 672 848**

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MAUAJI ya kutisha yanatokea ndani ya gesti moja maeneo ya Kigogo jijini Dar es Salaam. Mfanyabiashara Burhan anauawa ndani ya gesti ya Tukutane, akiwa na msichana mmoja mrembo aitwaye Mwanaidi. Polisi wanawakamata watu wote waliokutwa humo, pamoja na wafanyakazi wa gesti hiyo kwa ajili ya mahojiano. Lakini inaonekana muda ambao walikuwapo wapenzi hao hakukuwa na mteja mwingine yeyote zaidi yao.

Baada ya mahojiano ya kina, inaonekana kabisa kuwa Mwanaidi ndiyo muuaji. Je, ni kweli? Kwa nini alimuua mpenzi wake wakiwa wamejifungia chumbani? Fuatilia hadithi hii kwa makini ambayo mbali na kukutia simanzi, furaha na kukuburudisha, pia itakufundisha, elimu na kufunulia mambo ambayo hukupata kuyafikiria kabla.

# Lazima Apatikane-12

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

MARTIN aliongea na kuangalia saa yake ya mkononi, akiwa bado amekamatia bastola yake.

"Mkakati na akili ikabadilika, nikaona sasa Burhan nimuue kwa kisu ili wewe ndiyo ujulikane kama muuaji, kwa sababu nilijua utarudi baadaye na soda zako na kukuta maiti. Ningemuua kwa bastola, kipigo au kabali, askari polisi wengetia shaka kama wewe ndiye muuaji, kwani mwanamume jasiri kama yule hawezi kuuawa kwa kupigwa au kabali na mwanamke, lakini kisu ni rahisi kwa sababu wangehisi umeuawa alipolala usingizi kama wanavyoamini sasa. Bastola ingekuwa ngumu kwa sababu hujawahi kumiliki, hivyo wangemtafuta mtu mwingine, lakini hii ya kukung'ang'ania wewe nilifanya kwa makusudi. Aina ya kuuaji niliibuni ili kuwapoteza lengo polisi wakukamate wewe."

"Nilichofanya ulipoondoka tu ni kuingia ndani kiurahisi kwa sababu mlango haukufungwa. Alikuwa hajajiandaa kumuona mtu kama mimi. Alishtuka, lakini kabla hajafanya lolote nilimpiga ngumi ya uso akaangukia kitandani, nikammalizia kwa kumshindilia na kisu mara nne kifuani, niltoka bila kuonekana na yoyote yule mle ndani." Alinyamaza na kuonekana kama amemaliza au anasubiri yamuingie.

"Saa zimekwenda sasa, natakiwa nitoke hapa, kwa heri Mwanaidi." Alisema huku akiwa anakoki bastola yake, tayari kwa kuitumia. Ni wakati ambao Mwanaidi alikuwa amefumba macho akisubiri zawadi yake risasi cha kichwa kutoka kwa Martin.

Alisikia sauti kali. Sauti iliyotaka hata kuziba masikio yake. Ni sauti kama kuna kitu chuma au jiwe kubwa limepiga juu bati na kutoa mlio ya kutisha.

Alihisi kuwa huenda hiyo ndiyo sauti inayoashiria mtu anavyokata roho na kufa, akielekea kuzimu.

Alitaka kusema "Mama nakufa..." Lakini sauti haikutoka.

Sekunde kadhaa zilipita. Alijiona kama mtu anayeanguka kutoka kwenye shimo refu lenye kina kirefu kisicho na mwisho.

Alisikia vishindo vingine kadhaa vilivyozidi kuchanganya na asijue kuwa bado yupo duniani, au tayari ameshawasili ahera.




"Pumbavu wewe." Ni sauti aliyoisikia kwa mbali kama anaota hivi.

"Hivi unadhani ungeendelea kuua tu kirahisi kila unavyojiskia ee. Leo ndiyo mwisho wako."

Woga na mwili kukosa nguvu ulimfanya Mwanaidi ahisi hayupo duniani tena. Tayari alijua ameshauawa kutokana na sauti kali ambazo hakupata kuzisikia kabla.

Wakati wote huo alikuwa amefumba macho na mikono yake pia kuiziba usoni ili asishuhudie kifo chake kwa macho.

Taratibu alifumbua macho yake ili kuangalia kama atakutana ana kwa ana kitu gani huko ahera. Hakuamini alichokiona.

Badala ya kuwa ahera alijikuta bado yupo nyumbani kwake. Yupo kwenye chumba chake kile kile ambacho sekunde chake zilizopita alikuwa ameelekezewa bastola, tayari kwa kuuawa.

Ndani na watu wawili tu na mlango ulikuwa umefungwa. Alikuwa ni yeye na Martin. Alichokiona sasa ni tofauti.

Ndani sasa mlikuwa na watu watatu. Aliongezeka mmoja.

Aliyeongezeka ni mtu ambaye anamfahamu. Ni mtu aliyempa dhamana ya kesi ya mauaji wa mpenzi wake Burhan. Ni Afande Jan John.

Alikuwa amekamata bastola yake, huku Martin aliye amenguka sakafuni, damu zikiwa zinamchuruzika.

Mdomo wa bastola ya Jan John ilimuelekezea Martin na alionekana kuwa makini ili asije kufanya chochote kile.

"Ukitikisika tu, bastola hii inakohoa na kutoa kitu ambacho kitaondoa uhai wako kama ulivyofanya kwa wenzako."

Mwanaidi hakuamini macho yake. Alione akama anaota moja ya ndoto bora sana ambazo ameshawahi kuota kwenye maisha yake.

"Afande Jan. Ni wewe?" Aliita Mwanaidi kwa sauti ya furaha, lakini iliyochanganyikana na uchovu.

"Ni mimi Mwanaidi. Nimekuja kukuokoa." Ni kama Mwanaidi alikuwa amerudiwa na fahamu zake na kutaka kutoka kitandani kwa lengo la kwenda kumkumbatia Jan.

Alitambua hilo. "Hapana Mwanaidi. Usitoke hapo na waka usiinue hata hatua moja. Huu ni wakati wa hatari zaidi. Huyu siyo jambazi wa kawaida. Ngoja kwanza tumalize hili."

Maneno yale yalimfanya atulie papale kitandani, lakini akiwa mtu aliyeanza kupata faraja na matumaini mapya kwenye maisha yake ambayo kwa karibia mwaka sasa yalikuwa yamegubikwa na mikasa mizito yenye utata, hatarishi na yaliyotishia kumfunga jela, kufungwa maisha, kunyongwa au kuuawa akiwa msichana mdogo tu mwenye miaka ya 25 tu.

**Taratibu alifumbua macho yake ili kuangalia kama atakutana ana kwa ana kitu gani huko ahera. Hakuamini alichokiona. Badala ya kuwa ahera alijikuta bado yupo nyumbani kwake. Yupo kwenye chumba chake kile kile ambacho sekunde chake zilizopita alikuwa ameelekezewa bastola, tayari kwa kuuawa.**

******************************

Sauti aliyoisikia Mwanaidi iliyofanana na kitu kama chuma au jiwe kubwa limepiga juu bati na kutoa mlio ya kutisha, haikuwa nyingine bali ni teke kali ya karate la Jan lililopiga mkono wa Martin ambao kidole chake kimoja kilikuwa kinajiandaa sasa kukamua kitufe ili auawe.

Ilikuwa kama mzimu, kabla Martin kufanye chochote, Jan alikuwa ameshamuwahi kwa teke hilo, na kabla hajajua nini kimetokea, alimpiga ngumi mbili kisogoni zilizomfanya kufanyanyikiwa, kabla ya kumshusha mtama wa nguvu uliomfanya kuanguka chini kama gunia. Wakati wote huo, Martin hakujua nini kimetokea, kwani hali hiyo ilitokea ghafla sana.

Mguu wa Jan ulitua kwenye taya la Martin akiwa chini na kusababisha damu zianze kumtoka mdomoni. "Ulidhani wewe ni mjanja sana unaweza kuendelea na upumbavu wako hadi mwisho wa dunia ee." Aliuliza Jan kwa kebehi.

"Kaka Jan huyo ndiye aliyemuua Burhan, wala siyo mimi. Kasema mwenyewe hapa."

"Usiwe na wasiwasi Mwanaidi. Wala usidhani mimi nimeingia humu sasa hivi. Umeona pale mlango umefunguliwa?""Hapana."

"Umeona labda juu kumefumuliwa nimeingia?"

"Hapana kaka."

"Basi usiwe na wasiwasi. Kila kitu alichokisema au alichokwambia tangu mwanzo, nimekisikia kuliko wewe unavyodhani."

Mwanaidi alimuona Afande Jan ni kama malaika aliyeshushwa juu kutoka kwa Mungu, siyo kumuokoa na kifo kutoka kwa Martin tu, lakini pamoja na kumuondolea balaa la kesi ya mauaji dhidi ya Burhan ambayo ushahidi wote hadi wa kimazingira ulionyesha yeye ndiye muuaji.

"Mwanaidi, nimerekodi kila kitu, kwa hiyo hakuna kitu ambacho atabisha mbele ya sheria. Kwa sauti yake alichokuwa akiongea hapa akidhani kuwa anamhadithia mtu ambaye baadaye atamuua, mimi nilikuwa nyuma ya kabati lile nikarekodi vizuri kabisa."

Mwanaidi alishangaa na kusifu kimoyomoyo akili na utendaji wa afande Jan, ambaye tangu alipopewa faili lake alionekana yupo tofauti na wengine na kuanza kumhusudu.

ITAENDELEA JUMAMOSI

## HABARI MICHEZO




# THIAGO HARIDHISHWI NA KIWANGO CHAKE

**LIVERPOOL,** England

THIAGO Alcantara amekiri kutokuwa na furaha na kiwango chake na maswali yameendelea kuulizwa juu ya thamani yake pale Anfield.

Klopp alimnunua kiungo huyo mchezeshaji raia wa Hispania wakati wa majira ya joto mwaka 2020, baada ya kutoka kubeba mataji makubwa matatu akiwa na Bayern Munich. Lakini nyota huyo ameshutumiwa kwa sasa hayupo kwenye kasi yake ya uchezaji.

Thiago, hata hivyo, alicheza vizuri katika mechi ya ushindi wa mabao 2-0 ya Ligi ya Mabingwa Ulaya raundi ya 16 dhidi ya Leipzig huko Budapest, Jumatano.

Akikumbuka wakati wake akiwa Ujerumani, Thiago ameiambia: "Sisomi maneno juu ya kile watu wanazungumza juu yangu.

"Ninajua ninapata ukosoaji juu ya kiwango changu, lakini sina furaha na kiwango changu tangu nilipokuja hapa. "Klabu mpya, hali ya kushangaza, nilikuwa na jeraha kubwa, kwa hiyo kuingia kwenye kuzoea mchezo ilikuwa ngumu, lakini sio kisingizio."

# Klopp: Liverpool haiwezi kushinda Uefa

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesema kuwa licha ya ukweli kwamba kila timu inashiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa nia ya kushinda taji hilo, bado haoni nafasi ya timu yake kufanya hivyo msimu huu.

Klopp amesema hayo baada ya mchezo wa hatua ya 16 bora uliopigwa katika dimba la Anfield, Liverpool ikishinda mabao 2-0 dhidi ya RB Leipzig, juzi.


Mabao ya Mohamed Salah na Sadio Mane yalifanya matokeo ya uwiano kuwa 4-0 na sasa Liverpool wanasonga mbele katika hatua ya robo fainali ikiwa ni mara ya tatu katika miaka minne.

"Sababu ya kushiriki mashindano haya ni kushinda, lakini msimu huu kwetu hauonekani kama wa kushinda taji hili," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari.

"Sidhani kama Liverpool kwa sasa ina nafasi hiyo, kwani inaonekana wazi kuwa jambo hili ni gumu kwetu.

"Ingawa nina imani na wachezaji wangu, lakini ukweli lazima usemwe, kwa sasa hayupo kwenye nafasi nzuri ya kushinda taji hili."




# Maguire agoma kuomba radhi mashabiki

**MANCHESTER,** England

NAHODHA wa Manchester United, Harry Maguire, amegoma kuomba msamaha kwa kushindwa kufunga bao kwenye mchezo wa Ligi ya Europa hatua ya 16 bora dhidi ya AC Milan, juzi Alhamisi.

Beki huyo wa kati alikwama kubadili nafasi aliyopata kwa kupiga mpira uliogonga mwamba na kufanya United ilazimishe sare ya kufungana bao 1-1 dhidi ya AC Milan ndani ya dimba la Old Trafford.

Amad Diallo alifunga bao dakika ya 50 kwa United na Simon Kiaer akasawazisha dakika ya 92 kwa Milan, hivyo kuwa na kibarua cha kusaka ushindi katika mchezo wa marudio unaotarajiwa kuchezwa Machi 18, mwaka huu.

Maguire amesema: "Nilipaswa kufunga, lakini kwa hilo siwezi kuomba msamaha kwa yoyote.

"Ndio maana mimi ni beki sio mshambuliaji, lakini hakuna jambo la kuomba msamaha ilipaswa nifunge.

Maguire ameongeza kuwa United inahitaji kucheza vizuri kwa ajili ya mchezo wao ujao San Siro wiki ijayo ili kupata ushindi.

HABARI MICHEZO

# Fernandes aitikisa Utd

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa Manchester United, Bruno Fernandes, ameripotiwa hayupo tayari kuongeza mkataba mrefu zaidi ndani ya kikosi hicho, kwa mujibu wa vyombo vya habari vya England.

United inataka kumwongezea mkataba wa miaka mitano mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno, ili kujiondoa kwenye presha ya kumpoteza.

Lakini nyota huyo amegoma kumwaga wino kwa sasa, hadi hapo atakapohakikishiwa usajili wa wachezaji bora zaidi ili kuwa na makali ya kufukuzia mataji hasa la Ligi Kuu England na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Tangu alipojiunga na United, Fernandes amekuwa moto akifunga mabao 35 na kutoa pasi za mwisho 21 katika mechi 63 za michuano yote aliyoitumikia miamba hiyo.

Fernandes mwenye umri wa miaka 26, alisaini mkataba wa miaka mitano na nusu ambapo analipwa pauni 100,000 kwa wiki wakati alipojiunga United akitokea Sporting Lisbon.

Na sasa miamba hiyo ya Old Trafford imempa ofa ya mkataba wa miaka mingine mitano na mshahara wake ukiongezeka kuwa pauni 200,000 kwa wiki.

Wiki iliyopita, kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer, aliwaambia mashabiki wa timu hiyo kuhusu dirisha lijalo la uhamisho wa majira ya joto kwamba, wasitarajie usajili mkubwa kutokana na hali ngumu ya uchumi.






# GUARDIOLA ATAJWA KOCHA BORA ZAIDI

**LONDON,** England

KOCHA wa Fulham, Scott Parker, amemtaja bosi wa Manchester City, Pep Guardiola kama mmoja wa makocha bora zaidi ambaye amewahi kuwaona.

Parker ametoa kauli hiyo kutokana na timu hiyo kuwa kileleni mwa Ligi Kuu England, huku wakishinda michezo 21 mfululizo katika michuano yote wanayoshiriki, kabla ya kupokea kipigo kutoka kwa wapinzani wao wa jiji moja Manchester United, Jumapili.

Raia huyo wa Hispania alinukuliwa siku za hivi karibuni akidharau mafanikio yake akisema City imekuwa moto huku ikiwa na wachezaji wa kawaida.

Aidha, Parker ambaye atakiongoza kikosi chake dhidi ya Manchester City leo kwenye mchezo wa Ligi Kuu, amemsifia kocha huyo huku akisema amejipanga vya kutosha katika kukabiliana na timu hiyo.

# *Mourinho: Ndombele, Kane kuivaa Arsenal*

**LONDON,** England

HARRY Kane alitolewa wakati wa mchezo dhidi ya Dinamo Zagreb kwenye Ligi ya Europa baada ya kuumia, lakini atakuwa fiti kwa kuwavaa Arsenal hapo kesho, kwa mujibu wa Kocha wa Tottenham, Jose Mourinho.

Kane alifunga mabao yote mawili katika ushindi wa 2-0 juzi Alhamisi katika mchezo wa kwanza wa hatua ya 16 bora katika dimba la Tottenham.

Mourinho alimtoa Kane wakati pia mchezaji, Tanguy Ndombele alitolewa mapema baada ya bao la pili kufungwa.

Lakini Mourinho anajiamini wote wawili watapatikana na kuwa tayari kwa ajili ya mchezo dhidi ya Arsenal.

Alipoulizwa kama kuna jambo lolote la kuzungumza kuhusu Ndombele, Mourinho aliiambia BT Sport: "Sidhani kama ninalo, hata kwa Harry, siamini kama kuna jambo lolote kubwa.

"Ujue kuna mechi ambayo kila mtu anataka kucheza na vitu vidogo haviwezi kwenda kuwazuia kucheza Jumapili, naamini watakuwa vizuri.

Kane ambaye alikuwa na mashuti matatu na kutengeneza nafasi mbili kwenye mechi ya juzi, sasa amehusika kwenye mabao sita (amefunga mara nne na kutoa pasi za mwisho mbili katika mechi mbili za Spurs zilizopita.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RAMOS AMPIGIA CHAPUO HAALAND

### Asema mshambuliaji huyo wa Dortmund ana sifa za ziada ukimlinganisha na Mbappe...

**MADRID,** Hispania

NAHODHA wa Real Madrid, Sergio Ramos, amesisitiza itakuwa rahisi zaidi kwa mabingwa hao wa LaLiga kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Haaland, badala ya nyota wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe.

**Mbappe amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka kwa mabingwa wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, PSG, kwenda Madrid, lakini nyota wa Dortmund, Haaland pia akitajwa kuwaniwa na timu hiyo.**

Haaland ni mchezaji anayewindwa zaidi akihusishwa na timu kama Barcelona, PSG, Manchester United, Manchester City, Chelsea, Liverpool na Juventus, baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia akiwa na Dortmund kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ramos anahisi Haaland anafaa zaidi kwa Madrid hasa kutokana na hali ya kiuchumi kwa sasa baada ya mlipuko wa virusi vya corona.

"Ningependa wote waje, lakini kama anatakiwa mmoja wao, itakuwa rahisi zaidi kumsajili Haaland," amesema Ramos, ambaye bado majaliwa yake hayajajulikana kama ataongeza mkataba hapo Madrid, akiiambia Ibai Llanos.

"Kwa Mbappe kutokana na tatizo la kiuchumi ni ngumu sana. Kwa Haaland sio mbaya kwa sababu atakuwa na njaa ya mabao... itakuwa rahisi kufikia makubaliano kwa Haaland."

Haaland aliweka rekodi ya kuwa mchezaji aliyefunga kwa haraka zaidi mabao 20 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya katika mechi 14, wakati Dortmund ilipotoka sare ya 2-2 na Sevilla Jumanne na kufuzu hatua ya robo fainali kwa ushindi wa uwiyano wa 5-4.

Akiwa na umri wa miaka 20 na siku 231, Haaland pia akawa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kufunga mfululizo kwenye mechi sita za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Huku pia akiwa mchezaji wa kwanza kwenye historia ya mashindano hayo kufunga mabao mawili katika mechi nne mfululizo.

Mbappe pia aliweka historia kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumatano baada ya PSG kuiondoa Barcelona kwenye hatua ya 16.

Fowadi huyo aliifikia rekodi ya Lionel Messi ya kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kufikisha mabao 25 kwenye mashindano hayo akiwa na umri wa miaka 22 na siku 80.

## ZISIKUPITE

### PSG YAMTAKA RONALDO

KLABU ya Paris St-Germain inafuatilia hali ya Cristiano Ronaldo kule Juventus na kuangalia uwezekano wa kumsajili mshambuliaji huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 36, ikiwa ataamua kuondoka Turin. ***(Le Parisien)***

### MESSI ANUKIA MAREKANI

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Lionel Messi (33), atacheza misimu miwili zaidi barani Ulaya, kabla ya kujiunga na Inter Miami ya Marekani, huku uwezo wa mchezaji huyo kuendelea kusalia Barcelona hata baada ya msimu huu ukibashiriwa kuwa kwa asilimia 50 - 50. ***(Cadena Ser)***

### COMAN KUMRITHI PULISIC

CHELSEA inamwania winga wa Bayern Munich, Kingsley Coman mwenye umri wa miaka 24, kama mwenye uwezekano wa kuchukua nafasi ya Christian Pulisic, wakati ambapo mchezaji huyo mwenye miaka 22 raia wa Marekani ataondoka Stamford Bridge. ***(Mail)***

### BOWAT LULU ENGLAND

ARSENAL, West Ham, Everton na Brighton zote zinawania kumsajili mlinzi wa Scotland, Ibane Bowat, mwenye umri wa miaka 18 kutoka Fulham. ***(TeamTalk)***

### DONNARUMMA KUSEPA

WAKALA wa Gianluigi Donnarumma, 22, Mino Raiola inasemekana alianza mazungumzo na Chelsea na Manchester United kuhusu mlinda lango huyo wa AC Milan. Mkataba wa mchezaji huyo utamalizika msimu huu. ***(Transfer Window Podcast, via Football London)***

### MATIC KURUDI BENFICA

KIUNGO wa kati wa Manchester United, Nemanja Matic, 32, amesema atafikiria kurejea Benfica ikiwa kuna atakayemhitaji, ingawa mchezaji huyo wa Serbia amesisitiza ana furaha Old Trafford. ***(Sport TV, via Sun)***

### JOSE KIMEELEWEKA

KLABU ya Wolves ina nafasi ya kufanya majadiliano ikiwa itaamua kufikia makubaliano ya kudumu na mshambuliaji wa Brazil, Willian Jose, 29, ambaye yuko kwa mkopo kutoka Real Sociedad. ***(Express and Star)***

### WIJNALDUM KUTUA BARCA

BARCELONA itatoa mkataba kwa kiungo wa kati wa Uholanzi, Georginio Wijnaldum, 30, ambaye anatarajiwa kuondoka Liverpool kwa uhamisho huru, wakati mkataba wake utakapomalizika mwisho wa msimu. ***(Football Insider)***

### INTER MILAN YAKWAMA

INTER Milan pia imefanya mazungumzo na wakala wa Georginio Wijnaldum, lakini yamekwama. ***(Calciomercato)***

### MAVROPANOS: SIONDOKI

MLINZI wa Arsenal, Konstantinos Mavropanos, 23, raia wa Ugiriki ambaye amemvutia Kocha wa Stuttgart wakati wa kipindi chake cha mkopo, hayuko tayari kuondoka kwa washikabunduki hao. ***(Bild, via Mirror)***

HABARI MICHEZO

# KMC FC YAOTA KUREJEA MASHINDANO YA AFRIKA

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Msaidizi wa KMC FC, Habib Kondo, amesema lengo la timu yake kwa sasa ni kurejea katika mashindano ya kimataifa kama ilivyofanya mwaka 2019 ilipofanikiwa kucheza michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

**Akizungumza baada ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi, Kondo alisema malengo ya klabu hiyo ni kumaliza katika nafasi nne za juu na kujiweka katika nafasi ya kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa.**

"Mwanzoni kila timu inakuwa na lengo la kutwaa ubingwa. Lakini ligi inapozidi kwenda kila timu inaanza kujua nafasi yake iko wapi. Hata sisi ni hivyo hivyo. Kwa sasa akili yetu ni kumaliza kwenye nafasi nne za juu ambazo zinawezekana kabisa zitakuwa na faida msimu huu, nafasi zinaweza kuongezeka," alisema Kondo.

Kuhusu mechi yao dhidi ya Ruvu Shooting, kocha huyo alisema ilikuwa ngumu lakini iliamriwa kutokana na wachezaji kufuata maelekezo waliyotoa.

"Wale waliozidi au kutimiza kwa usahihi maelekezo ya walimu ndiyo walifanikiwa kutoka na ushindi," Kondo alisema.

Hata hivyo Kondo alisema timu yake imekuwa ikipata tabu kwenye viwanja vya ugenini kwa kupoteza michezo na kuvuna pointi tatu wanapocheza kwenye Uwanja wa Uhuru, aliweka wazi inasababishwa na viwanja vingi vya mikoani kutokuwa kwenye ubora.

"Sisi tunacheza mpira wa chini, sasa tukienda ugenini tunapata tabu na viwanja. Vingi havipo kwenye hali nzuri na wachezaji wetu inabidi watumie nguvu zaidi kupambana," aliongeza kocha huyo.

KMC kwa sasa inakamata nafasi ya tano ikiwa na pointi 35 baada ya kucheza michezo 24 huku vinara wa ligi hiyo wakiwa ni Yanga yenye pointi 50 wakifuatiwa na mabingwa watetezi, Simba yenye pointi 46, lakini ina viporo vitatu.

KMC ilipata nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa mwaka 2019 baada ya Tanzania kutoa timu nne kwenye michuano ya CAF na katika msimamo wa Ligi Kuu Bara wao walimaliza katika nafasi ya nne huku Azam FC iliyokuwa nafasi ya tatu ikibeba Kombe la FA.

## Kisubi afunguka kuidhibiti Simba

**Na Saada Akida**

GOLIKIPA chaguo la kwanza wa Tanzania Prisons, Jeremiah Kisubi, amesema siri kubwa ya timu yake kuvuna pointi nne dhidi ya Wekundu wa Msimbazi msimu huu imetokana na kuwasoma vyema mabingwa hao watetezi na kufahamu udhaifu.

Kisubi alisimama langoni katika mechi zote mbili dhidi ya Simba msimu huu, ya kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga ilimalizika kwa wenyeji kushinda bao 1-0 wakati waliwalazimisha vigogo hao wa Kariakoo sare ya goli 1-1 wakiwa ugenini.

Kisubi aliliambia gazeti hili walijipanga kwa ajili ya kupata matokeo mazuri hivyo walipambana kuhakikisha hawapotezi mchezo huo muhimu katika hatua hizi za lala salama.

Kisubi alisema Simba ni timu nzuri kwa sana hali ambayo waliingia kwa tahadhari kubwa na heshima dhidi ya wapinzani wao ili kuhakikisha wanapata matokeo chanya.

Aliongeza tayari wamefunga hesabu za mechi hiyo na wanajipanga kwa ajili ya mechi ijayo dhidi ya JKT Tanzania itakayochezwa mjini Sumbawanga.

## Azam kuwanoa zaidi mastraika

**Na Saada Akida**

LICHA ya kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Ihefu FC, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema bado wana kazi ya kuwakumbusha washambuliaji wao kuongeza umakini wanapokuwa jirani na lango la wapinzani.

Vivier alisema wamepata matokeo mazuri lakini washambuliaji wake wanashindwa kutumia nafasi nyingi wanazozitengeneza, hivyo wanatakiwa kuwa makini zaidi.

"Tunatengeneza nafasi nyingi za mabao, mfano dhidi ya Mwadui FC, lakini hata mechi ya leo (juzi) dhidi ya Ihefu FC nayo tumetengeneza nafasi zaidi ya saba, lakini tumefanikiwa kupata tatu," alisema Vivier.

Naye Kocha Mkuu wa Ihefu FC, Zuberi Katwila alisema matokeo mabaya ambayo timu yake imepata yanampa wakati mgumu katika vita ya kusalia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

"Tuna wakati mgumu sana wa kupambana katika mechi 10 zilizobakia, ukizingatia tuko katika nafasi ya 16 ni mbaya katika msimamo," alisema Katwila.

Alisema kutokuwa makini kwa wachezaji wake na kutowaheshimu wapinzani wao imekuwa sababu kubwa ya kupoteza michezo ya ligi hiyo iliyoko katika hatua ya lala salama ingawa aliwapa mbinu mpya za kuwazuia Azam FC.




Promota wa pambano la uzito wa Light linalotambuliwa na Shirikisho la Ngumi la Kimataifa la WBF, Evarist Ernest (katikati), akionyesha mkanda utakaowaniwa katika pambano litakalofanyika Machi 19, mwaka huu. Kushoto ni bondia Mtanzania Twaha Kiduku na Jones Segu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## *Kiduku, Kayembe kuzipiga Dar*

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA maarufu nchini, Twaha Kiduku, anatarajia kupambana na Mkongomani Tshibangu Kayembe katika pambano la kimataifa la uzito wa Super Welter lililopangwa kufanyika Machi 19, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Ubungo Plaza jijini Dar es Salaam.

Pambano hilo limeandaliwa na promota Evarist Ernest wa Kampuni ya Mopao Entertainment na kabla ya hapo bondia, Jones Segu atatetea mkanda wake wa WBF wa uzito wa Light dhidi ya Hanock Phiri kutoka Malawi.

Akizungumza jijini jana, Ernest alisema maandalizi ya pambano hilo yamekamilika na mabondia wote kutoka nje ya nchi watawasili nchini Jumatatu.

"Tshibangu Kayembe alipambana na Hassan Mwakinyo kuwania mkanda wa WBF kwenye ukumbi wa Mlimani City na kupigwa kwa pointi. Anakuja kulipiza kisasi kwa Kiduku ambaye anataka kurejesha hadhi yake baada ya kupoteza pambano nchini Misri hivi karibuni," alisema Evarist.

Kiduku alitamba atamchapa mpinzani wake kabla ya raundi 10 kumalizika.

"Nimejiandaa vyema na lengo langu ni kushinda kwa knockout (KO), Kayembe ni bondia mzuri sana, anajua kuzipanga ngumi zake, nitakuwa makini wakati wote," alisema Kiduku.

Pambano lingine litakalofanyika siku hiyo litakuwa ni kati ya Halima Bandola na Najma Isike ambao watachuana katika uzito wa Light raundi nne.

# Michezo

Jumamosi Machi 13, 2021

Nipashe



Ramos ampigia chapuo Haaland UKURASA 22

# GOMES AGEUKIA MABEKI SIMBA SC

## Barbara ateta na Infantino, afunguka Africa Super League yanukia...

**Na Saada Akida**

UKUTA! Ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kuondoka na ushindi, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, amesema atafanya mabadiliko katika safu yake ya ulinzi kuelekea mechi ya Kundi A ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Merreikh kutoka Sudan itakayochezwa Jumanne kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

**Katika mechi hiyo ya marudiano, Simba itawakosa wachezaji wake wawili, Pascal Wawa na Taddeo Lwanga kutokana na kutumikia kadi za njano.**

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Gomes alisema uamuzi wa kufanya mabadiliko katika safu hiyo umetokana na nyota waliokuwapo awali kulazimika kukaa nje kwa mujibu wa kanuni lakini kwake ni sehemu ya kuendeleza kukiimarisha kikosi chake. Gomes alisema safu ya ulinzi ya mechi iliyopita ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Tanzania Prisona inatoa taswira ya kikosi chake huku akiendelea kuwapa mbinu mpya mabeki watakaoziba nafasi za Wawa na Lwanga.

"Tunaendelea na maandalizi ya mechi ijayo dhidi ya Al Merreikh, tunaendeleza kufanyia kazi upungufu wetu, tunajua mchezo utakuwa wa ushindani mkubwa baada ya kuangalia mechi ya Al Ahly dhidi ya AS Vita, nina imani tunatakiwa kutumia vizuri uwanja wa nyumbani ili kupata matokeo chanya katika mchezo huo," alisema Gomes.

Kocha huyo aliongeza anaridhishwa namna wachezaji wake wanavyoendelea kujituma kuanzia mazoezini hadi kwenye mechi na hamasa hiyo inamwongezea nguvu ya kufikia malengo.

"Wana viwango na ari nzuri, ninawaona moja kwa moja na wanavyojituma, wanajaribu kufuata vizuri maelekezo ninayowapa mazoezini na kuyahamishia uwanjani, hii inatusaidia kupata matokeo chanya, bado tuko vizuri," Gomes alisema.

Mfaransa huyo alisema malengo makubwa ya Simba ni kuhakikisha inaongeza umakini na kushinda mchezo huo wa nne na kuendelea kuongoza kwenye kundi lao na kukaribia hatua ya robo fainali.

Simba inaongoza katika msimamo wa Kundi A ikiwa na pointi saba ikifuatiwa na AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) yenye pointi nne sawa na Al Ahly ya Misri huku Al Marreikh nayo ikiwa na pointi moja.

Wakati huo huo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, amekutana na Rais wa Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), Gianni Infantino na kubadilishana mawazo mbalimbali yanayohusu mchezo huo.

Barbara amepata nafasi hiyo akiwa nchini Morocco ambapo alikwenda kama mgeni mwalikwa kwenye Mkutano Mkuu wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), uliokuwa unaendelea jijini Rabat.

"Ulikuwa ni wasaa mzuri wa kukutana na Rais wa Fifa, Gianni Infantino, pembezoni mwa mkutano wa uchaguzi wa CAF. Maandalizi ya kuanza kwa African Super League yanaendelea," alisema Barbara.

Ligi hiyo inayotarajiwa kufanyika kuanzia wakati wowote msimu ujao itashirikisha vilabu 20 vikubwa vya barani Afrika na itasaidia kutangaza vipaji vya nyota wa mataifa ambayo yatashiriki.



Rais wa Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), Gianni Infantino (kulia), akiwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Barbara Gonzalez, kwenye Mkutano Mkuu wa Uchaguzi wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), uliofanyika jijini Rabat, Morocco jana. **PICHA: MTANDAO**

## Mwambusi aandaa hesabu za ubingwa

**Na Mwandishi Wetu**

KAIMU Kocha Mkuu wa Yanga, Juma Mwambusi, amesema yuko tayari kupambana na kuipa heshima na furaha klabu hiyo ambayo imeukosa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa misimu mitatu mfululizo.

Mapema wiki hii, mabosi wa Yanga walitangaza kumrejesha Mwambusi kwenye kikosi hicho baada ya kuachana na aliyekuwa Kocha Mkuu Mrundi Cedric Kaze.

Mwambusi aliliambia gazeti hili alitarajia kukutana na kikosi chake kwa mara ya kwanza jana jioni na amepanga kuandaa programu maalumu kutokana na baadhi ya nyota kuwa kwenye majukumu ya timu za taifa.

Kocha huyo alisema ameanza kazi yake akiwa na wachezaji wachache lakini anaamini kwa muda huu ambao Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama, atayafanyia kazi masuala ya kujiimarisha kimbinu na kila mmoja kufahamu kwa usahihi majukumu yake kulingana na nafasi anayocheza.

"Kwa sasa hakutakuwa na jipya kwa sababu naanza mazoezi leo (jana), nimekuwa na wachezaji wachache sana kwa sababu wengi wameitwa katika timu za taifa, na wachache kupewa ruhusa ya mapumziko mafupi, suala la mbinu litakuwa baada ya wachezaji wote kurejea," alisema Mwambusi.

Aliongeza kwa sasa afya yake imeimarika kwa asilimia 90 na amefanya uamuzi wa kurejea kuifundisha Yanga baada ya kuruhusiwa na daktari wake.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042